

**RONALDINHO AKANUSHA KUIPONDA BRAZIL** UK. 22


# Nipashe

Jumatatu Juni 17, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581710

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US www.twitter.com/nipashetz

www.ippmedia.com www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper



**YALIYOMO**

UKURASA WA 5

**Lori** lagonga basi na kuua watu wanne



UKURASA WA 8

**Mtambo** mwingine Bwawa la Nyerere wawashwa ukizalisha umeme MW 235



UKURASA WA 8

KANUNI MPYA:

**Ukitenda** mambo haya wakati wa uchaguzi ujue gereza linakuita




SIKU YA MTOTO WA AFRIKA

# Walioko mahabusu ya watoto waanika madhila ya kutisha

• **JINAI** ya ulawiti, mauaji, bangi yaponza wengi, malezi duni kiini cha tatizo; Rais Samia acheza nao Ikulu... *Endelea Ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akisherehekea Siku ya Mtoto wa Afrika akiwa pamoja na wajukuu, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. Siku hii huadhimishwa Juni 16 ya kila mwaka. **PICHA: IKULU**

## Mchango wa ununuzi gari la Tundu Lissu wafikia mil 76/-

UK. 5

RIPOTI MAALUM

## Ndoto ya Nyerere yazimwa


• **Kiwanda** chake cha zana za kilimo chageuzwa cha mabomba ya maji; maumivu kwa wakulima... *Uk. 4*

**Na Mwandishi Wetu**

NDOTO ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere kuhakikisha Tanzania inajitosheleza kwa zana za kilimo, imezimwa.

Kiwanda cha zana za kilimo alichojenga mwaka 1970, hivi sasa hakizalishi zana hizo, bali ...


**MICHEZO** **MUKOKO: YANGA BINGWA TENA 2024/2025** UK.24 **KATUNI** UK.6




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kamuzu, Lilongwe nchini Malawi, anatarajiwa kumwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika mazishi ya kitaifa ya aliyekuwa Makamu wa Rais wa Malawi, Hayati Dk. Saulos Chilima, jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

SIKU YA MTOTO WA AFRIKA

# Walioko mahabusu waanika madhila

**Na Restuta James**

WATOTO wanaokutwa na makosa ya kukinzana na sheria wanakabiliwa zaidi na jinai ikiwamo ubakaji, ulawiti, mauaji, wizi na uvutaji bangi na sigara.

Hayo yalielezwa jana na watoto wanaopewa malezi na marekebisho ya tabia katika mahabusu ya watoto iliyoko Upanga, jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika.

Wakizungumza kupitia ngonjera, watoto hao walisema chanzo ni malezi duni ya familia, huku wakieleza kuwa ndani ya mahabusu hiyo wanapata ushauri, unasihi na mafunzo ya ujuzi yanayowawezesha kuwa raia wema wanaporejea uraiani.

Watoto hao walisisitiza umuhimu wa elimu jumuishi kwa watoto wote izingatie maarifa, maadili na stadi za kazi.

Baadhi ya watoto ambao wamefanyiwa marekebisho ya tabia na sasa wako uraiani, walisema mabadiliko ya tabia yamefanya jamii iwakubali na kuwaamini baada ya kutoka mahabusu.

Mwanaisha Nasoro alisema alifikishwa katika mahabusu hiyo Septemba mwaka jana na alitoka mwezi uliofuata baada ya kesi yake kumalizika, akiwa amepata ujuzi wa kushona nguo ambao anautumia hivi sasa.

"Ninatoa wito kwa watoto na vijana wenzangu kwamba wafanye kazi kwa bidii na wasichague kazi, mradi ni kazi halali na waache tamaa hata kama wanalipwa ujira kidogo. Wasione aibu kufanya kazi au vibarua halali," alisema.

Mwanaisha alishauri wazazi na walezi kupunguza kupiga watoto mara kwa mara kwa kuwa wanajenga usugu kwa watoto wao.

mahabusu, alifundishwa namna bora ya kuishi na jamii, jambo ambalo limemfanya akubalike aliporejea uraiani.

"Sasa ninamsaidia mama yangu kazi zote za nyumbani. Ninajua kupika, kulima, kufanya usafi na zaidi nina tabia nzuri. Ninashauri vijana tujifunze kuwajibika na tuepuke makundi," Felix alisema.

Chacha Marwa alisema alikaa mahabusu hiyo kwa miezi minne na nusu kwa kosa la jinai na sasa amekuwa raia mwema baada ya kufanyiwa unasihi.

"Sasa hivi ninalima na ninaishi nyumbani kwa amani. Ninashukuru viongozi wa hapa kwa namna walivyonisaidia kurekebisha tabia yangu," alisema.

Hata hivyo, Chacha alisema anakabiliwa na changamoto ya kiuchumi baada ya hali mbaya ya hewa kuharibu mazao yake shambani.

Naye Nuru Abdallah alishauri vijana kuwasikiliza wazazi na kuepuka makundi.

Awali Meneja wa Mahabusu hiyo, Darius Damas, alisema watumishi kituoni huko wanafanya kazi ya kurekebisha watoto tabia kwa kuwafanya wajutie makosa yao, wabadilike na wakubali kuwajibika katika jamii.

Alisema takwimu zinaonesha kwamba watoto wa kiume ndio wanaokabiliwa zaidi na makosa kulinganishwa na wa kike.

"Mahabusu ina uwezo wa kuhudumia watoto 50 wa kiume na wa kike 10, lakini tangu nimeanza kazi hapa miaka mitano iliyopita, hatujawahi kuwa na watoto sita wa kike kwa mara moja. Hata leo tuna watoto 13 na miongoni mwao wa kike ni mmoja tu," alisema Damas.

Meneja huyo alisema changamoto kubwa ya kuwafanya watoto wakinzane na sheria ni malezi duni ndani ya familia, ikiwamo kuwanyima baadhi ya haki za msingi kama vile chakula.

Alisema mahabusu inakabiliwa na miundombinu mibovu ya majitaka na majengo yake kuezekwa mabati ya asbestos yaliyopigwa marufuku, hali inayohatarisha afya zao.

Katibu wa Jumuiya ya Maridhiano na Amani Tanzania (JMAT), Sheikh Yassin Masenga, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika maadhimisho hayo, alisema wazazi na walezi wanapaswa kusimamia wajibu wa malezi ya watoto kimwili na kiroho ili kuwaepusha kulelewa na mifumo mingine.

Alisema desturi ya maisha na elimu ya dini ni maarifa ambayo familia zinapaswa kuwafundisha watoto mapema ili wakue wakimjua Mungu.

Kuhusu changamoto za mahabusu, alisema JMAT kwa kushirikiana na wadau wake itazifanyia kazi.

Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ni 'Elimu Jumuishi kwa Watoto Izingatie Maarifa, Maadili na Stadi za Kazi.'

Sheria ya Ulinzi wa Mtoto ya Mwaka 2009, pamoja na mambo mengine, inaelekeza wazazi, walezi na jamii kuhakikisha watoto wanapewa haki zao za msingi ambazo ni pamoja na elimu, chakula, kucheza na kudekezwa.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
15.06.2024

TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe 16.06.2024 hadi 22.06.2024 kampuni ya CEVA Interfreight itasafirisha mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka Bandari ya Dar Es Salaam kuelekea Mzenga, gari hilo lenye namba za usajili

**NRB97300 / NRB54202 & DS00TG GP / NRB53910**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

**Urefu - Mita 28.00**
**Upana - Mita 7.30**
**Kimo - Mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: Bandari ya Dar Es Salaam hadi Mzenga kupitia Barabara ya Mandela, Barabara ya Morogoro mpaka Mlandizi, magari yatasafiri muda wa usiku ( Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri). Kutoka Mlandizi kwenda Mzenga magari yatasafiri muda wa mchana ( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*


## ...Rais asherehekea Siku ya Mtoto wa Afrika na wajukuu

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika kwa kualika watoto kutoka sehemu mbalimbali nchini kisha kusherehekea nao kwa michezo, kuchora na kutembelea Ikulu ya jijini Dar es Salaam.

Siku ya Mtoto wa Afrika huadhimishwa Juni 16 kila mwaka. Kwa Tanzania kaulimbiu ni 'Elimu Jumuishi kwa Watoto Izingatie Maarifa, Maadili na Stadi za Kazi'.

Lengo la maadhimisho hayo ni kukumbusha juhudi zinazofanywa kunyanyua mtoto wa Afrika na changamoto zinazotokea kuhakikisha anapata elimu bora.

Katika kuadhimisha siku hiyo jana, Rais Samia alisisitiza umuhimu wa serikali, familia na jamii kushirikiana kuhakikisha watoto wanapata malezi bora yenye maadili mema.

Rais Samia alihimiza kuhakikisha usalama wa mtoto unakuwa jukumu la jamii nzima na siyo mzazi tu, pia akasisitiza kuwapatia elimu na historia za kuwahimiza uzalendo kwa nchi yao tangu wakiwa wadogo.

Watoto hao walipata muda wa kujifunza mambo mbalimbali kuhusu nchi yao pamoja na kuburudika na michezo ya aina tofauti. Video fupi iliyowekwa katika ukurasa wa mtandao wa kijamii wa Instagram wa Ikulu, ilimwonyesha Rais Samia akiwaongoza watoto hao kuchora picha ya Bendera ya Taifa huku akiwatia moyo na kuwapa motisha.

Rais pia alifundisha watoto kuhusu Ikulu kwa kuwauliza maswali ili kujua ufahamu wao kuhusu ofisi hiyo kuu nchini kisha kuwaelekeza pale alipoona wanahitaji ufafanuzi.

"Hapa ni wapi? Ikulu au Posta? Ikulu anakaa nani? Ikulu hakai Mama Samia wala Bibi Samia, Ikulu anakaa Rais," alisema.

Baada ya kumaliza shughuli za nje, Rais aliwapeleka ndani ya jengo la Ikulu na kuwatembeza sehemu mbalimbali, ikiwamo ofisini kwake.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dorothy Gwajima, alimshukuru Rais Samia kwa kutenga muda wake kusherehekea na watoto na kuhimiza wazazi kujenga utaratibu wa kutenga muda wa kukaa, kuzungumza na kucheza na watoto wao. Kupitia ukurasa wake wa Instagram, waziri huyo aliandika, "Shukrani Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutenga muda wako na watoto kwenye Siku hii ya Maadhimisho ya Mtoto wa Afrika."

HABARI KITAIFA

# Serikali yasuka mpango mageuzi sekta ya mifugo

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amesema serikali imeandaa mpango wa mageuzi ya sekta ya mifugo utakaosaidia kupata ufumbuzi wa changamoto zinazokabili sekta hiyo nchini.

Dk. Biteko aliyasema hayo jana wilayani Kibaha, Pwani wakati akifunga maonesho na mnada wa mifugo kwa mwaka 2024.

"Wizara msichoke wala msiache kuwapa elimu wafugaji wetu, lazima tukubali kuwa wamekuwa hivyo kwa miaka mingi, mabadiliko lazima yatokee na lazima tujue kuwa maeneo mengi yanayohitaji ardhi yanaongezeka, ikiwa ni pamoja na mifugo lakini ardhi haiongezeki.

"Hivyo, tuendelee kuwapa elimu ya ufugaji kisasa na kuhimiza wafugaji waje kwenye maonesho kama haya ili wapate ujuzi na teknolojia itakayowasaidia," aliagiza Dk. Biteko.

Dk. Biteko aliwataka wafugaji wasijione dhaifu wala wanyonge, akitolea mfano kuwa unaweza kukuta mfugaji ana ng'ombe 1,000, huwezi kumuita maskini kwa kuwa ng'ombe hao wanaweza kuwa mtaji; kinachohitajika ni namna anavyoweza kubadilisha maisha yake kwa kutumia hao ng'ombe alionao.

Naibu Waziri Mkuu huyo alisema kuwa ni vyema maonesho hayo ya mifugo yakafanyika kikanda ili kuwafikia wakulima wengi zaidi nchini, ikiwa ni pamoja na kuwasaidia kupata ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili kama vile mbegu bora za mifugo au kujua teknolojia za kisasa za ufugaji.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti, alipongeza washiriki na wadhamini wa maonesho hayo ya mifugo ambayo yanalenga kutoa elimu kwa wafugaji ili kuleta tija.

"Maonesho haya ni ya muhimu na kwa mwaka huu tumeyawekea nguvu zaidi kwa kuwa yanaleta matokeo makubwa na kwa kuwa yamekuwa maelekezo ya viongozi wetu wa serikali kuwa wafugaji wetu wasifuge kizamani.

"Lazima sasa ifike mahali wafugaji wetu waondokane na ufugaji wa kizamani kwa mwamvuli wa kimila, na sisi wizara tumekuwa tukitoa elimu mara nyingi kupitia wataalamu wetu na maofisa ugani licha ya wafugaji hawa kuwa na mwamko mdogo wa kufuga kisasa," alisema Mnyeti.

Alitolea mfano kuwa wafugaji hutembea umbali mrefu kutafuta malisho na matokeo yake mifugo inafika ikiwa imechoka na kuwa serikali imeendelea kutenga maeneo ya malisho ili kusaidia wafugaji nchini.

"Tunatoa elimu ya kufuga kisasa kwa kunenepesha mifugo na kuuza hata ng'ombe mmoja kwa Sh. 500,000 au zaidi badala ya Sh. 200,000. Wafugaji lazima wajue ng'ombe ambaye hajafugwa kisasa, hajapata chanjo au akiugua anapewa tu dawa kiholela, hawezi kuuzwa nje ya nchi kwa sababu hana ubora," alisema Mnyeti.

# Wizara Zanzibar, USAID washirikiana kukuza matumizi ya nishati mbadala

**Na Mwandishi wetu,** ZANZIBAR

WIZARA ya Maji, Nishati na Madini kwa kushirikiana na Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) kupitia Mpango wa Power Africa imeendesha mafunzo ya nishati mbadala Zanzibar.

Mafunzo hayo yamekutanisha wadau wa sekta ya utalii na kampuni binafsi za nishati kutokana na Shirika la Maendeleo la Kimataifa (USAID) kuunga mkono sekta ya utalii Zanzibar kwa kuhakikisha inaingiza mapato makubwa zaidi kwa uchumi.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na Ubalozi wa Marekani nchini, lengo lingine ni kuhakikisha sekta hiyo inapata nishati ya uhakika kwa ajili ya hoteli na fukwe zinazopokea maelfu ya wageni kila mwaka.

Warsha hiyo ilitoa fursa za matumizi ya nishati mbadala kwa sekta ya utalii Zanzibar ikiunganisha hoteli na kampuni zinazotoa huduma za nishati mbadala. Pia kulikuwa na majadiliano na uwasilishwaji mada kuhusu matumizi ya nishati mbadala nje ya Gridi ya Taifa.

"USAID na Power Africa zinafurahishwa na ushirikiano wa Serikali ya Zanzibar katika kuhimiza umuhimu wa matumizi ya nishati mbadala kwenye sekta ya utalii," alisema Plato Hieronimus, Naibu Mkurugenzi wa Ofisi ya Ukuaji wa Uchumi ya USAID/Tanzania.

"Tuna matumaini kuwa majadiliano yaliyofanyika kwenye warsha hii yataleta matokeo chanya ambayo Zanzibar inaweza kuyatumia kuweka mazingira wezeshi kwa maendeleo," aliongeza.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pia imebainisha uzalishaji nishati mbadala kuwa muhimu kwa ukuaji wa sekta hiyo, kutegemea vyanzo vya nishati mbadala kutahakikishia usambazaji umeme thabiti na wa bei nafuu kwa hoteli, ambazo zinaweza kuongezwa au kupunguzwa matumizi kulingana na misimu, na hivyo kuokoa gharama na rasilimali.

"Tunafurahia matumizi ya nishati mbadala kama chanzo cha nishati inayotumika katika hoteli zetu na kukidhi mahitaji ya sekta ya utalii," alisema Waziri wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Shahib Kaduara,

"Matumizi ya nishati mbadala yatazifanya hoteli zetu kuwa na nguvu, mwanga na kufanya kazi, jambo ambalo litaimarisha sekta ya utalii na uchumi wa Zanzibar," aliongeza.

Wakati dunia inashughulikia mahitaji ya nishati yanayoongezeka kila kukicha, pamoja na tishio la mabadiliko ya tabianchi, Zanzibar ina mikakati ya kufikia kujitegemea katika nishati kwa kuangalia fursa zinazopatikana kupitia nishati mbadala. USAID na Power Africa zinajivunia kukuza utumiaji wa vyanzo safi, vya bei nafuu na vya kutegemewa vya nishati.


Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Ndoto ya Mwalimu Nyerere yazimwa

## -Kiwanda chake cha zana za kilimo chageuzwa cha mabomba ya maji; maumivu kwa wakulima...

**Na Mwandishi Wetu**

NDOTO ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere kuhakikisha Tanzania inajitosheleza kwa zana za kilimo, imezimwa.

Kiwanda cha zana za kilimo alichojenga mwaka 1970, hivi sasa hakizalishi zana hizo, bali kinazalisha mabomba ya maji.

Mnamo Machi 4, 1970, serikali chini ya uongozi wa Rais Nyerere, ilianzisha kiwanda cha zana cha kilimo UFI (Ubungo Farm Implements) kilichoko Shekilango, wilayani Ubungo, Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Cleopa Msuya, aliyekuwa Waziri wa Viwanda wakati huo, lengo la kujenga kiwanda hicho ni kuhakikisha zana za kilimo zinapatikana nchini kwa bei nafuu wakati wote pasi na vikwazo.

Msuya anasema uanzishaji wa kiwanda hicho ni utekelezaji wa sera za kuendeleza viwanda muhimu nchini ambazo ni silaha muhimu za kupiga vita umaskini kwa kupunguza kutegemea zana za kilimo kutoka nje ya Tanzania.

Zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania wanategemea kilimo kuendesha maisha yao, huku sekta hiyo ikichangia asilimia 26.5 katika Pato la Taifa na asilimia 65 ya malighafi za viwanda nchini. Hii ni kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Kilimo za mwaka 2023/24.

Sekta ya kilimo ikiwa tegemeo kwa maisha ya karibu robo tatu ya wananchi, kiwanda hicho cha kwanza cha zana za kilimo kujengwa nchini, hiki sasa hakizalishi tena zana za kilimo kwa ajili ya wananchi. Zana hizo zinaingizwa nchini na wafanyabiashara wanaozitoa China, India na kwingineko ughaibuni.

Wakati dhamira ya Mwalimu Nyerere na serikali yake ilikuwa wananchi wawe na uhakika wa kupata zana hizo nchini na kwa bei nafuu, wakulima waliozungumza na mwandishi wa habari hii wanasema zana hizo sasa zinauzwa bei ghali na wakati mwingine baadhi hazina ubora.

Ni hali inayofanya mazingira ya kilimo kwa wakulima wadogo ambao ndio wengi zaidi nchini kuwa magumu, hivyo kukinzana na dhamira ya Mwalimu Nyerere ya kuinua uchumi wa wananchi kupitia kilimo.

Kamati ya Kufuatilia Mafao ya Wafanyakazi 508 wa UFI inasema kiwanda hicho kilikuwa maarufu kwa kutengeneza majembe ya mkono, mapanga, majembe ya kukokotwa na wanyama, makwanja na zana nyinginezo za kilimo.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Ally Killindo anasema kiwanda hicho kimepata mwekezaji mpya kutoka China, Tianjin Machinery Import and Export Group, ambaye hazalishi zana za kilimo, bali mabomba makubwa ya maji.

"Wakati kiwanda kinafanya kazi na hadi tunasimamishwa tulizalisha zana nyingi sana, maghala yalikuwa yamejaa.

"Ghafla wakaanza kusema hakuna masoko licha ya kwamba wafanyakazi tulikuwa tunayaona masoko ya zana hizo kwenye maeneo mengi nchini kwa kuwa kilimo kilitegemewa sana.

"Hadi sasa wakulima wanahangaika kupata zana za kilimo kwa kuwa zinaagizwa nje na watu binafsi ambao hujipangia bei," anasema Killindo.

Katibu wake, Makamba Kigome anasema wameandika barua na kuwaisilisha kwa Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson wakiwa na malalamiko ya kutolipwa stahiki zao zaidi ya Sh. bilioni moja ambazo ni malimbikizo ya mishahara, likizo, nauli, kodi ya nyumba na mafao. Barua iliwasilishwa ofisini kwa Spika Februari 14 mwaka huu.

"Tumeitumikia nchi yetu kwa juhudi, maarifa na weledi wa hali ya juu na kuiwezesha serikali kupiga hatua katika sekta ya kilimo. Tuliendelea kufanya kazi hadi Julai 31, 1998, serikali ilipokabidhi kiwanda kwa kampuni ya China ya Tianjin Machinery Import & Export Group kwa njia ya ubinafsishaji," inasomeka sehemu ya barua hiyo ambayo mwandishi ameona nakala yake.

Katibu Killindo, aliyekuwa mfanyakazi wa UFI, anasema kiwanda kilizalisha zana zote muhimu za kilimo ambazo ni pamoja na majembe, mashoka, mapanga, plau, jembe palizi, jembe la matuta, na jembe la kupandia, kikiwa na matawi mjini Musoma na Mbeya.

Kwa ufupi, Killindo anasema aina 28 za zana kilimo zilitengenezwa na UFI, zikijumuisha pia visu vya kuvunia, haro, sululu, ndimi za plau, kabali, makwanja, beleshi, rato, koleo, minyororo, plau ya ardhi tifutifu, plau la kugawa matuta, mipini, plau la kupandia, mikasi, mashine za kupukuchulia, mikasi ya kuchongea, makoa na vifaa vyake, reki, nyundo, uzio na teso.

Mwandishi wa habari hii amebaini kuwa mashine zote zilizokuwa zinatumika kutengeneza zana za kilimo katika kiwanda hicho zimeng'olewa na hakuna taarifa rasmi juu ya zilikopelekwa.

Vilevile, mwandishi pia anafahamu kwamba kiwanda hicho kilijengwa kwa msaada wa Serikali ya China kutokana na uhusiano wa kidiplomasia uliopo kati ya Tanzania na nchi hiyo.

Hata hivyo, mkataba baina ya pande zote mbili haukuwahi kuwa wazi; Julai 1998 Serikali ya Tanzania ilikabidhi kiwanda kwa kampuni ya China ya Tianjin Machinery Import & Export Group kwa ajili ya ubinafsishaji.

Mwandishi amebaini kuwa ubinafsishaji ulifanywa kwa matarajio ya kuboresha uzalishaji na kuingiza teknolojia mpya ya zana za kilimo.

Hata hivyo, imebainika kuwa mwekezaji mpya kutoka China, baada ya kukabidhiwa kiwanda, aliendelea kutengeneza zana za kilimo kwa muda mfupi kisha akageukia utengenezaji mabomba ya maji huku sehemu kubwa ya majengo ya UFI ikigeuzwa kuwa ghala la bidhaa kutoka China.

Mwandishi anafahamu kuwa kwa hivi sasa kiwanda hakitengenezi tena zana za kilimo, bali kinazalisha mabomba kwa ajili ya miradi ya maji.

Mmoja wa wafanyakazi wa kiwanda cha mabomba ya maji (jina tunalo) anasema, "baada ya kiwanda kubinafsishwa, baadhi yetu tulibaki hapa (kiwandani). Mwekezaji aliyechukua hakuendelea na uzalishaji zana za kilimo, anazalisha mabomba ya maji.

"Wengi wetu tupo hapa tangu mwaka 2009. Kiwanda kilianza uzalishaji mabomba mwaka 2016. Mwekezaji mpya alipoingia, aliondoa mfumo wa mashine za majembe na kufunga mfumo wa mabomba na baadhi ya mashine zilibaki zikaendelea kutumika, zikiwamo za kuchonga vipuri.

"Mwekezaji alianza kuendesha kiwanda kwa kuzalisha mabomba, wakati huo ilikuwa ni kwa ajili ya mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kuyapeleka Shinyanga.

"Wakati kiwanda cha UFI kinafanya kazi, Watanzania ndio tulifanya kazi, hata kwenye masoko kama Kariakoo tulikuwa na maduka ya kuuza zana za kilimo, tulifurahi kupata riziki. Cha kushangaza ni kuwa licha ya kufanya kazi kwa miaka 20, niliambulia Sh. 600,000 tu," anadai.

Mwandishi alimtafuta Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, kutaka kujua sababu za kiwanda kutozalisha tena zana za kilimo, hasara iliyopata serikali kutokana na kiwanda kubadilishwa matumizi na uwabikaji wa waliochangia kiwanda kutotekeleza jukumu lake la msingi.

Hata hivyo, Juni 2 mwaka huu, Waziri Mkumbo ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Ubungo aliahidi kujibu maswali hayo baadaye, lakini akitanguliza maelezo ya awali kwamba kiwanda hicho kilishafungwa. Hadi sasa hakuna maelezo zaidi ya waziri huyo juu ya kiwanda hicho.




Mwonekano wa majengo ya kilichokuwa Kiwanda cha Zana za Kilimo UFI (Ubungo Farm Implements), yaliyopo upande wa kushoto mwa Kituo cha Mwendokasi Shekilango, barabara ya Morogoro. Kwa sasa ni kiwanda cha mabomba cha TSP Limited (Tanzania Steel Pipe). Chini ni mwonekano wa zamani wa kiwanda hicho. **PICHA: MTANDAO**




***Itaendelea kesho**



Baadhi ya wanachama wa Chama cha ACT-Wazalendo wakiinua mikono kuunga mkono msimamo wa kutaka uchaguzi wa serikali za mitaa usimamiwe na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wanaochangia ununuzi gari la Lissu wafikisha milioni 76/-

**Na Jenifer Gilla**

MCHANGO wa fedha za kumnunulia gari Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, umefikia Sh. milioni 76.7 kati ya Sh. milioni 300 zinazohitajika kumnunulia gari kiongozi huyo.

Fedha hizo zimetolewa na wadau hao ndani ya siku 24 tangu kuanzishwa harambee hiyo, ikiwa wa wastani wa Sh. milioni 3.2 kwa siku.

Lissu alithibitisha kufikisha kiasi hicho cha fedha kupitia mtandao wake wa X siku tatu zilizopita, akihamasisha wafuasi wake kuendelea kumchangia ili lipatikane gari kwa ajili ya kuendelea na shughuli zake za siasa.

"Kwa upendo, wema na ukarimu wenu gari jipya litapatikana, hili (lililoshambuliwa kwa risasi mwaka 2027) itawekwa makumbusho ya mapambano ya kidemokrasia nchini kwetu na kazi ya ukombozi itaendelea," aliandika Lissu.

Mei 17, mwaka huu, wafuasi wa mwanasiasa huyo wakiongozwa na mwanaharakati Maria Sarungi, waliazimia kumchangia Sh. milioni 300 mtaalamu huyo wa sheria anunue gari jipya ili lile la zamani ambalo lilishambuliwa kwa risasi, lihifadhiwe kwa ajili ya ukumbusho.

Mei 18 mwaka huu, Lissu alikabidhiwa gari lake aina ya Toyota Land Cruiser V8, VXR na Jeshi la Polisi jijini Dodoma, baada ya kupita miaka saba tangu aliposhambuliwa kwa risasi na watu wasiojulikana nyumbani kwake Area D, Septemba 7, 2017. Baada ya kukabidhiwa gari hiyo, Lissu alieleza lengo lake la kulitengeneza ili aendelee kulitumia katika shughuli zake za kisiasa mpaka pale litakapochoka, jambo ambalo wafuasi wake walipinga na kusisitiza watamnunulia gari jipya ili hilo liwe ukumbusho juu ya kile kilichompata.

Ndani ya saa 48 tangu Maria aweke namba za malipo kwa ajili ya kukusanya fedha hizo kupitia mitandao ya kijamii ya X na Instagram, zilikusanywa Sh. milioni 15, jambo lililoonesha dhamira ya dhati ya wafuasi wa mwanasiasa huyo.

Katika ukurasa wake wa X, Maria anaendelea kuhamasisha wafuasi na wapenzi wa kiongozi huyo kuchanga ili kiasi hicho cha fedha kipatikane na gari linunuliwe kwa muda waliopanga.

## Lori la mchanga lagonga basi, laua abiria wanne

**Na Steven William,** MUHEZA

WATU wanne wamefariki dunia na wengine wanne kujeruhiwa baada ya lori kuligonga kwa nyuma gari dogo la abiria aina ya Nissan Caravan.

Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Tanga, Willy Mwamasika, amethibitisha kutokea kwa ajali hiyo saa tatu usiku wa kuamkia jana katika Kijiji cha Tanganyika, wilayani Muheza, mkoani Tanga.

Akizungumza na mwandishi wa habari jana, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Maketi Msangi, alisema kuwa ajali hiyo ilihusisha basi dogo la abiria Nissan Caravan lenye namba T228 DTD na lori aina ya Volvo lenye namba T 925 CAU ambalo lilikuwa limebeba mchanga kuelekea mjini Tanga.

Alitaja watu waliopoteza maisha ambao walikuwa abiria kwenye basi kuwa ni Kondakta Anuari Juma (30), Shani Omari na Hassan Abdallah (mmoja alikuwa hajatambuliwa) huku majeruhi wanne wakipelekwa kupatiwa matibabu katika Hospitali Teule ya Muheza.

Akifafanua kuhusu tukio hilo, Kamanda Msangi, alisema chanzo cha ajali ni basi dogo kupata hitilafu na kumlazimu dereva kulisimamisha pembeni.

Alisema kuwa wakati amesimama, anakagua basi hilo abiria waliteremka na kondakta wakawa wamesimama pembeni mwa basi hilo, ghafla lilitokea lori hilo likagonga basi kwa nyuma na kusababisha vifo na majeruhi.

Alisema dereva wa lori la mzigo, Elvice Livingston alitoroka baada ya ajali na kukimbilia kusikojulikana. Miili ya marehemu imehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhi maiti cha Hospitali Teule Muheza.

# TCRA yajipanga kudhibiti uhalifu fedha mtandaoni

**Na Mwandishi wetu,** ARUSHA

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imesema inaendelea kuweka jitihada za kupambana na kudhibiti uhalifu mitandaoni, ikiwamo huduma za kifedha kutokana na kuongezeka mifumo mipya ya mawasiliano ya teknolojia.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki jijini Arusha na Meneja wa Huduma za Posta wa TCRA, Cecilia Mkoba, wakati akizungumza katika jukwaa la wakurugenzi wakuu 42 wa Posta na taasisi za udhibiti mawasiliano waliokutana kuweka mipango ya maendeleo ya Sekta ya Posta Barani Afrika (PAPU).

"Nchi yetu tuna bahati kwamba hatujapata uhalifu kwenye sekta ya fedha na tunachoangalia ni kwamba tutaendeleza uelewa wa wananchi kwa sababu TCRA ni mwezeshaji katika mitandao, ili kudhibiti vitendo hivyo na kuvizuia," alisema.

Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania, Maharage Chande, alisema kadiri maendeleo ya teknolojia yanavyozidi kukua na shughuli za posta zilizokuwa zinafanyika awali zinapungua na hivyo wanakutana kuweka mikakati ya jinsi Bara la Afrika linavyoweza kutumia teknolojia kuboresha huduma za posta ikiwamo duka mtandao, usafirishaji na kuongeza ubunifu.

"Wiki hii tumeanza mikutano, mmoja ni huu wa mazungumzo ya kiposta ambao kikubwa tutamzungumzia teknolojia na jinsi itakavyoboresha huduma za posta.

Pia tutaangalia jinsi kanuni zitasaidia sekta ya posta kukua zaidi," alisema.

Chande alisema kuwa katika eneo la teknolojia, Tanzania imepiga hatua; Shirika la Posta limeanza kutoa mafunzo ya usimikaji mifumo ya kiposta kwa mataifa mengine ambako wataalamu kutoka Tanzania wanatumika katika nchi mbalimbali barani la Afrika kubadilishana uzoefu kwenye shughuli hizo.

"Mfano leo tumepokea wataalamu wetu waliokwenda kufundisha na kusimika mifumo Zimbabwe. Tanzania kwenye mtandao tuko mbele.

Hivi sasa katika mafunzo na usimikaji mifumo ya kiposta, wataalamu wetu wanatumika katika Bara la Afrika kufanya shughuli hizi," alitamba.

Akizungumzia changamoto za sekta ya posta na usafirishaji barani Afrika, Mjumbe wa Bodi ya Tume ya Mawasiliano Uganda, Paul Odoi, alitaja changamoto hizo ni pamoja na ongezeko la matumizi ya teknolojia, akisisitiza kuwa matumizi ya teknolojia yakizingatiwa yatasaidia kukuza sekta hiyo.

Kikao hicho ni mwendelezo wa Mkutano wa 42 wa Baraza la Utawala la Umoja wa Posta Afrika (PAPU), uliofanyika kwenye makao makuu ya umoja huo.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Yanga wanastahili pongezi na kuigwa

**MWEZI** uliopita tulishuhudia historia nchini katika anga la michezo hususani mchezo wa mpira wa miguu ikiandikwa baada ya Yanga kutangaza ubingwa wao wa 30 wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ni ubungwa wa tatu mfululizo ndani ya miaka mitatu wakipokea kijiti cha ubingwa kutoka kwa Simba waliotawala kwa misimu minne mfululizo.

Yanga imekuwa na mafanikio makubwa kwenye misimu hiyo huku ikafanya vizuri pia kwenye mashindano ya kimataifa, ikitinga fainali ya Kombe la Shirikisho msimu uliopita na hatua ya robo fainali ya Klabu Bingwa Afrika msimu huu.

Mafanikio hayo ya Yanga hayakufikiwa kimiujiza; imefika hapo kutokana na uwekezaji mzuri na bora, ikiongozwa na viongozi wenye maono mapana kwenye soka.

Hakuna ubishi uongozi wao chini ya Rais Hersi Said umesaidia kufika walipofika sasa na kushinikiza mafanikio waliyonayo sasa.

Pamoja na upinzani na ubishani wa kimichezo, Yanga wanastahili pongezi na kuwa mfano kwa klabu nyingine katika kufikia mafanikio waliyonayo sasa.

Zipo klabu nyingi ambazo zinapaswa kuiga mfano wa Yanga kwenye kujiendesha, usajili na hata maandalizi yao kuelekea msimu husika wa mashindano.

Mafanikio waliyonayo Yanga katika kipindi cha miaka mitatu yanatokana na uongozi bora pamoja na mwekezaji mwenye kiu ya mafanikio.

Rais wao ni kiongozi kijana mwenye maono, tamaa na kiu ya mafanikio na ndio maana hata akapigiwa kura kuwa Mwenyekiti wa Vilabu vya Soka Afrika.

Kwa viongozi wengine, si vibaya kuiga na kuwa na kiu ya mafanikio haya waliyofikia Yanga chini ya Hersi na sekretarieti yake.

Kwa uongozi wake na uimara wa klabu hiyo, haitashangaza kusikia msimu ujao wametwaa tena ubingwa wa Ligi Kuu na kufika mbali kwenye michuano ya Afrika.

Tusidanganye, uongozi imara na uchumi madhubuti wa klabu ndio kichocheo kikubwa cha mafanikio kwenye soka.

Timu nyingine zinapaswa kuiga mafanikio haya ya Yanga ambayo hata hivyo hayajaja mara moja, ni mchakato ulioanza miaka minne nyuma kabla ya kuchukua ubingwa kutoka kwa Simba.

Wakati Simba wakiwa kwenye kilele cha mafanikio, Yanga walikuwa wanakuna kichwa kuona ni namna gani wanaweza wakafikia mafanikio ya watani.

Baada ya mchakato huo wa muda mrefu, Yanga wamekuwa vizuri kwenye michuano ya ndani na nje. Kwa mara ya kwanza msimu uliopita tumeshuhudia timu hiyo ikicheza hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya milongo mingi.

Msimu mmoja nyuma, Yanga hiyo hiyo ilishuhudiwa ikicheza fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika. Haya ni mafanikio makubwa.

Tusibeze mafanikio haya, kuna kila sababu ya kuwapongeza Yanga hususani viongozi wao kwa kile wanachokifanya. Klabu nyingine ziige njia za viongozi wa Yanga kwenye kuiletea timu mafanikio.




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wanaotoa maoni Simba wanafungiwa, wanaoshusha 'brandi' wao wanaachwa

Na Adam Fungamwango

**NILIANDIKA** wiki iliyopita kuwa kosa walilofanya viongozi wa Simba ni kutowajibika kuita wanachama wao ili kuwaambia kinachoendelea wakati timu inafanya vibaya katika mechi za Ligi Kuu na Kombe la FA.

Lakini walipogusiwa kwenye maslahi yao ya kutaka kujiuzulu, wakaitisha vikao ambavyo si rasmi kwa ajili ya kile kilichoonekana kujihami.

Nikaandika kwa nini hawakufanya hivyo awali wakati timu inafanya vibaya, kwa sababu angalau wangeshusha presha ya wanachama na mashabiki wao.

Kilichoonekana ni kwamba baadhi ya viongozi wa Simba ni kama hawaangalii sana heshima, mafanikio na 'brandi' ya klabu, badala yake wanajiangalia wao tu.

Moja ya sifa ya kuongozi ni kuipandisha thamani klabu, kuitetea na kuilinda nembo, nguvu na gharama zote, baadaye ndiyo unaweza sasa kujiangalia mwenyewe.

Naona hilo limejirudia tena na sitolinyamazia, niliongelee tena ili kuwakumbusha uongozi wajibu wao ni upi ndani ya klabu.

Juzi Sekretarieti na klabu ya Simba imetangaza kuwafungia kujihusisha na masuala ya klabu wanachama wawili, Mohamed Khamisi Mohamed, maarufu kama Dk. Mohamed, na Agnes Daniel, maarufu kama Aggy Simba mpaka pale Kamati ya Maadili ikapoamua vinginevyo.

Sekretarieti ikadai imepokea malalamiko mengi ya kimaadili dhidi ya wanafamilia hao wa klabu, ikiwamo kuitisha mikutano kinyume na taratibu na kuchochea migogoro klabuni. Mwisho ikasema itawafikisha wanachama hao mbele ya Kamati ya Maadili hivi karibuni. Wala sipepesi macho nikisema haya yote yanatokea kutokana na sakata la kushinikizwa kujiuzulu kwa wajumbe upande wa wanachama.

Binafsi sikubaliani na adhabu hii kwani imekuwa kubwa mno, tofauti na kile ambacho walikuwa wanahitaji kukifanya wanachama hao.

Hawa walikuwa katika harakati za kutaka kuijenga Simba kutokana na kile kilichotokea cha kufanya vibaya kwa timu, iliyokuwa inaongozwa na viongozi hao ambao hadi leo hawajaitisha mkutano kuwaambia sababu ya kufanya vibaya msimu uliomalizika.

Mimi sidhani kama walikuwa wanachochea mgogoro, bali walikuwa katika harakati za kutoa maoni yao kama wanachama na mashabiki ili yafanyiwe kazi na uongozi, pamoja na malalamiko ni kwa nini timu ilifanya vibaya, kipi kilisababisha usajili uwe mbovu, na watajikwamuaje kutoka hapo.

Nadhani baadhi ya viongozi walichofanya ni kujilinda wao wenyewe, sidhani kama walikuwa na haja ya kufanya hivyo zaidi ya kuwaita na kuongea nao kwa sababu wote ni Wanasimba wanaojenga nyumba moja tu.

Hawa hawa akina Aggy Simba ndiyo wanaosafiri na timu kila inapokwenda ndani na nje ya nchi kuishangilia na kuwapa hamasa wachezaji, leo hii wanaonekana wanachochea migogoro, ambayo haipo.

Ndiyo wanaokusanya pesa na kuwasaidia matibabu baadhi ya wanachama na Simba waliopata ajali mbili, Machi 28, walipokuwa wanatoka mikoani kwenda Dar es Salaam, kutazama mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati ya timu yao ikicheza dhidi ya Al Ahly ya Misri.

Hawa wanaojitolea yote haya ndiyo wanaopewa adhabu hii ya kufungiwa.

Kama kuchukua hatua, nadhani sektetarieti ingefanya hivyo kwa baadhi ya wanaojiita wanachama na mashabiki wa Simba ambao wanashinda mitandaoni kuitukana, kuidhalilisha, kuiponda, kushusha hadhi na 'brandi' ya klabu.

Hawa mbona hatujawahi kuona angalau wakipata onyo, au kuchukuliwa hatua kwa sababu moja kwa moja wanaiharibu nembo ya Simba.

Wanavaa jezi za Simba, lakini hawana chochote kizuri ambacho timu yao inafanya. Aggy na Dokta Mohamed wanaonekana wanaongea kwa uchungu. Lakini hawa wengine wanaonekana wanaongea kwa kejeli, dharau na udhalilishaji uliovuka mipaka. Sijaona viongozi wakidili nao kisheria ili wathibitishe kwanza kama wao ni wanachama au mashabiki wa Simba kama wanavyojinasibu, halafu mengine yafuate.

Na kwa nini wavae jezi za klabu na kuidhalilisha? Kama ni mashabiki wa timu nyingine waliojificha kwenye kivuli hicho, basi wavae jezi zao. Badala yake wamekaa kimya tu.

Hii ina maana hawatumii nguvu kuitetea nembo ya klabu, au kuilinda, ukiharibu 'brandi' ya Simba kwao sawa tu, wanaonekana hawana mpango na hilo, ila ukigusa maslahi yao ndipo wanapotumia nguvu na mamlaka walizopewa na klabu ili kujilinda wao binafsi. Kwa nini wasifanye hivyo pia kuilinda klabu yenyewe ya Simba dhidi ya wanaochafua nembo?

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

**HABARI KITAIFA**

# Mtaala waandaliwa kufundisha ualbino

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKURUGENZI wa Kinga Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Crispin Kahesa, amesema wanaandaa mtaala maalum wa elimu kwa ajili ya kupeleka shuleni ili kufundisha juu ya ualbino na vitu vinavyotakiwa kuzingatiwa.

Kahesa aliyasema hayo mwishoni mwa wiki mjini Kibaha alipozungumza na waandishi wa habari, akibainisha kuwa ili walimu wajengwe uwezo, lazima kuwe na mtaala maalum.

Pia alisema mtaala huo utakuwa shirikishi kwa kuelimisha kuhusiana na kujikinga, kugundua na matibabu. Vyote hivyo vitakuwa kwenye mfumo wa kusaidia kuondoa hatari ya kupata saratani ya ngozi.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, katika kila watu 2,500 nchini, mmoja ana ualbino na kati ya watu wanne wenye ualbino, mmoja yuko kwenye hatari ya kupata saratani ya ngozi.

"Kutokana na hali hiyo tumeona kuna haja kufikisha elimu kwa jamii na shuleni kufanya uchunguzi wa awali sambamba na kuandaa mtaala maalum utakaokwenda kufundishwa shuleni," alisema.

Kahesa alisema kuwa katika kutoa elimu shuleni wamekuwa wanashirikisha Chama cha Watu Wenye Ualbino (TAS) ambao wanaainisha shule zenye watoto wenye ualbino na kufikisha elimu huko.

Elimu inayotolewa na taasisi hiyo ni pamoja na athari zinazosababisha saratani ya ngozi, shughuli wanazotakiwa kufanya, nguo za kuvaa na dalili za awali za mabadiliko ya ngozi.

Wakiwa mjini Kibaha mwishoni mwa wiki, watu wenye ualbino waliomba serikali kuongeza nguvu kudhibiti ukatili unaoendelea dhidi ya kundi hilo sambamba na kuwaongezea ulinzi wakati wa mchakato wa uchaguzi.


Uzoefu unaonesha matukio ya ukatili dhidi yao yanakuwa mengi wakati wa mchakato wa uchaguzi wa kitaifa.

Katika kilele cha Siku ya Kimataifa ya kuongeza uelewa kwa watu wenye ualbino, serikali ilitoa maagizo kwa halmashauri zote nchini kutenga bajeti kwa ajili ya kununua mafuta ya watu wenye ualbino.

Maagizo hayo yalitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Pwani Abubakar Kunenge, alipomwakilisha Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Deogratias Ndejembi kwenye maadhimisho hayo.

Mkuu wa Mkoa alipongeza jitihada za serikali kutengeneza mafuta ya watu wenye ualbino, jambo ambalo ni hatua kubwa.

Maboresho yanaendelea kukidhi mahitaji ya walengwa nchini.



Shekhe wa Kata ya Tingeni wilayani Muheza mkoani Tanga, Hamisi Said Samata (kulia), akisoma dua ya kuwakumbuka marehemu katika makaburi ya familia ya Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini, Balozi Adadi Rajabu (wa pili kulia), yaliyopo Kijiji cha Kerenge jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# 'Urutubishaji wa chakula uanzie ngazi za vijiji kukabili udumavu'

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameitaka mikoa yenye viwango vikubwa vya upungufu wa damu na udumavu nchini ianze kutekeleza mpango wa urutubishaji chakula kuanzia ngazi ya vijiji ili baada ya miaka mitano ijayo, zaidi ya nusu ya Watanzania wawe wanatumia chakula kilichorutubishwa.

"Hatua hii itachochea kasi ya kupungua kwa vifo vya kinamama wanaojifungua pamoja na watoto wachanga kutokana matatizo yanayohusiana na upungufu wa damu mwilini na kupungua kwa kinga mwili. Vilevile, itapunguza matatizo ya vichwa vikubwa na mgongo wazi kwa watoto," alisema Majaliwa juzi.

Waziri Mkuu alikuwa anazindua kiwanda cha kutengeneza virutubishi na tovuti ya wasindikaji chakula Tanzania kilichoko Mikocheni, Dar es Salaam. Ni kiwanda cha kwanza kwa Afrika Mashariki na cha pili barani Afrika.

Alisema kuwa ili kulinda afya za walaji, wasindikaji wote wazingatie namna ya kutunza virutubishi na vinyunyizi vya virutubishi ili visiharibike.

Waziri Mkuu aliagiza Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na wadau wote wa lishe, washirikiane kuandaa mkakati mahsusi wa kuelimisha umma na kuhakikisha wananchi wanapata uelewa mpana wa umuhimu wa virutubishi vinavyochanganywa kwenye chakula katika kukabiliana na changamoto za lishe duni.

Alisema uzinduzi wa kiwanda hicho ni sehemu ya mkakati mpya wa juhudi za serikali na washirika wake katika kuwezesha usindikaji bora zaidi na uwekaji virutubishi kukidhi mahitaji ya mwili.

"Urutubishaji huo utaendelea kupunguza viwango vya vifo vya kinamama wanaojifungua pamoja na vifo vya watoto wachanga vinavyotokana na matatizo yanayohusiana na upungufu wa damu mwilini," alisema.

Waziri Mkuu alisema urutubishaji huo utaimarisha afya ya watoto wa kike walio katika rika balehe kwa kuwapunguzia changamoto ya upungufu wa damu.

Alisema urutubishaji huo pia utasaidia kuimarisha afya za watoto kwa kukabiliana na tatizo la kupungua kinga mwilini ambalo ni chanzo cha watoto kuugua mara kwa mara pamoja na kupunguza matatizo ya vichwa vikubwa, mdomo sungura na mgongo wazi kwa watoto.

Akizungumzia kuhusu uzinduzi wa tovuti ambayo ni mahsusi kwa ajili ya mtandao wa wasindikaji wote wa chakula hasa unga na mafuta ya kula, Waziri Mkuu alisema una manufaa makubwa kwa kuwa pamoja na mambo mengine, unakusudiwa kutumika katika kutoa elimu na kuongeza ujuzi kutoka kwa wasindikaji wakubwa waliobobea kwenye teknolojia ya usindikaji chakula nchini na kwingineko duniani.

"Vilevile, ni fursa nyingine nzuri kwa wasindikaji kujiendeleza kwani nimearifiwa kuwa kupitia tovuti hiyo, wasindikaji wataunganishwa na wafadhili na kupata misaada mbalimbali. Misaada hiyo itawawezesha kuboresha mifumo ya usindikaji pamoja na uhakiki wa ubora na viwango vya virutubishi katika chakula," alisema.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alisema kuwa hadi sasa, mikoa yote 26 ya Tanzania Bara ina wazalishaji na wafungashaji unga wa mahindi 1,282 wanaoongeza virutubishi katika bidhaa hiyo.


Alisema hatua hiyo imefikiwa kwa ushrikiano na wadau wa lishe hasa wanaosaidia afua hiyo ya urutubishaji vyakula. Katika bajeti ya 2023/24, Wizara ya Afya ilitenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vinyunyizi 300 vya virutubishi wakati wa kusaga nafaka husussan unga wa mahindi na ngano na kufungwa katika vinu 300 vya halmashauri mbalimbali nchini.

"Kwa mwaka huu mpya wa fedha 2024/25, tumetenga kiasi cha Sh. bilioni moja katika bajeti yetu kuendelea kununua tena vinyunyizi ili urutubishaji uifikie jamii kubwa zaidi na kupunguza matatizo ya lishe niliyoyataja hapo juu," alisema.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe alisema suala la kuimarisha lishe kupitia uongezaji virutubishi viwandani limekuwa linafanyika kwa viwanda vikubwa tu tangu mwaka 2013, hasa kwa viwanda vya kuzalisha unga wa ngano na mafuta ya kula.

Aliongeza kuwa hivi sasa serikali inaendelea na jitihada za kuhakikisha wazalishaji wadogo nao wanaongeza virutubishi kwa kuwa kwa asilimia zaidi ya 80 ndio wanaolisha watu wengi zaidi. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga alimhakikishia Waziri Mkuu kwamba wataendelea kushirikiana na wadau katika kuratibu mpango wa lishe ili suala hilo liendelee kupewa kipaumbele.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed





Msimamizi wa Jumuiya ya Mabohora, Saifuddin Jamali (wa nne kulia), akichinja mbuzi ikiwa ni sikukuu ya Eid El Adh"haa ( Eid ya kichinja) inayoadhimishwa baada ya waumini wa kiislam kukamilisha ibada ya Hijja, hafla iliyofanyika jijini Dar as Salaam jana. Wa pili kulia ni Msimamizi Huzeifa Saifuddin. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mtambo namba nane Bwawa la Julius Nyerere wawashwa

**Na Joseph Mwendapole**

MTAMBO namba nane wa kuzalisha umeme katika Bwawa la Julius Nyerere umekamilika na umeshaanza kuzalisha umeme, ukiingiza megawati 235 kwenye Gridi ya Taifa.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati akizindua taarifa za utendaji katika sekta ndogo ya umeme, gesi asilia na mafuta kwa mwaka 2022/23 jijini Dodoma.

Alisema kuwa hivi sasa, jumla ya Megawati 470 zinazalishwa kutoka bwawa hilo na tayari zimeingizwa kwenye Gridi ya Taifa.

Akizungumzia sekta binafsi, Dk. Biteko alisema imeisaidia serikali kwenye mafuta, gesi na hata kwenye uzalishaji umeme, akitoa wito kwao kuchangamkia fursa zote zinazotokea.

"Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati, ninawaomba waangalieni watu wa sekta binafsi kama wadau muhimu wa maendeleo badala ya kuwaona kama washindani, wapendeni na wapeni ushirikiano," aliagiza Dk. Biteko.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Felchesmi Mramba, alisema tathmini iliyofanyika, inaonesha sekta ya nishati imepiga hatua kwenye maeneo mengi ikiwamo uhakika wa upatikanaji umeme, upatikanaji na usambazaji wa mafuta.

Alisema taarifa ya Benki ya Dunia (WB) kwa nchi zinazoendelea, inaonesha kuwa sekta ya nishati kwa Tanzania inafanya vizuri zaidi kulinganisha na nchi zote zinazoendelea na Bara la Afrika kwa ujumla.

Mramba alisema eneo lililofanya vizuri zaidi ni usambazaji umeme vijijini na miradi mingine ya nishati kama Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP).

Aliongeza kuwa WB imeidhinisha Tanzania kupatiwa Dola za Marekani milioni 300 ili kuendeleza umeme kutokana na ufanisi huo.

Akitoa taarifa za utendaji katika sekta ya nishati, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA), Dk. James Andilile, alisema sekta ya nishati inaendelea kuimarika ikiwamo uwekezaji kwenye miundombinu ya umeme.

Alisema uwekezaji umeongezeka katika uzalishaji, usafirishaji na usambazaji, upotevu wa umeme unazidi kupungua. Wateja wa umeme wameongezeka kutoka milioni 3.8 mwaka 2021/22 hadi milioni 4.4 mwaka 2022/23.

Dk. Andilile alisema changamoto zilizoainishwa kwenye taarifa hiyo katika sekta ya umeme ni uchakavu wa miundombinu ambao unaendelea kufanyiwa kazi kwa ukarabati wa miundombinu na uwekezaji endelevu.

# Ukifanya haya wakati wa uchaguzi gereza linakuita

**Na Christina Mwakangale**

WATENDAJI wanaoghushi taarifa, kuwa mdanganyifu, kuazimisha kadi kwa mwingine pamoja na kuharibu ujumbe uliobandikwa, ni makosa ambayo adhabu yake ni faini au kifungo gerezani au vyote kwa pamoja.

Hayo yamo katika Kanuni za Uboreshaji Daftari la Kudumu la Wapigakura Mwaka 2024 zilizofafanuliwa kwa mkoani Dar es Salaam kwa waandishi wa habari wakati wa mkutano ulioandaliwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC).

Katika kanuni hizo, sehemu ya tisa inataja makosa na adhabu; kifungu cha 52 hadi 58 vinaainisha adhabu hizo kwa mtendaji anayeandikisha kwa udanganyifu, anahamisha au anasababisha kuhamasisha taarifa yoyote ya uandikishaji.

Adhabu hizo pia zinatolewa kwa mtendaji au mtu anayetoa kwa mtu kadi ya mpigakura kinyume cha ilivyoelekezwa na kanuni hizo.

Anakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua Sh. 100,000 na isiyozidi Sh. 300,000 au kutumika kifungo kisichopungua miezi sita gerezani na kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Kifungu cha 53 cha kanuni hizo kinaelekeza, "mtu yeyote ambaye ataghushi, anafuta au kwa nia ovu anaharibu taarifa za kuandikishwa, atakumbana na adhabu hiyo."

Adhabu kama hiyo pia inatotolewa kwa anayechapa au kusambaza zana yoyote ya uandikishaji bila idhini ya tume au ofisa mwandikishaji.

## Akerwa ucheleweshaji ujenzi maktaba ya chuo

**Na Munir Shemweta,** TABORA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Punda amekerwa na kuchelewa kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa maktaba ya Chuo cha Ardhi Tabora (ARITA) kutokana na baadhi ya vifaa kutopelekwa kwa mzabuni.

Pinda ameelezwa na mkandarasi wa mradi huo, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kuwa ujenzi wa mradi huo ungekamilika kwa wakati, lakini kuchelewa kwa baadhi ya vifaa kwa ajili ya ukamilishaji ujenzi wa mradi huo kumesababisha mkandarasi kushindwa kutekeleza kazi yake kwa wakati.

"Kazi hii tungeweza kumaliza ndani ya siku 60 lakini changamoto kubwa ni vifaa, tumeshindwa kukamilisha kutokana na kuchelewa kufika kwa baadhi ya vifaa kwa wakati na hivyo kutufanya tushindwe kukamilisha kazi hii," alisema Meneja wa TBA Mkoa wa Tabora, Ebenezer Ngure.

Akizungumza wakati wa kukagua mradi wa ujenzi wa maktaba ya chuo hicho juzi, Naibu Waziri Pinda alimwagiza mkandarasi wa mradi huo kuandika ripoti inayoonesha mahitaji yote na kumfikia ifikapo Jumatano ijayo ili afanyie kazi changamoto zinazokwamisha ujenzi huo.

Awali uongozi wa chuo hicho ulimweleza Naibu Waziri Pinda kuwa kuna baadhi ya vifaa ambavyo Mkandarasi Mshauri ameomba vibadilishwe. Mzabuni aliombwa kwenda kuvichukua lakini hakufika, jambo lililomshangaza kiongozi huyo (Pinda).

Naibu Waziri Pinda aliagiza ubadilishaji vifaa kutoka kwa mzabuni kufanywa haraka kufikia kesho kwa kuwa wenye shida ni chuo, hivyo hawapaswi kusubiri mzabuni na badala yake chuo kifuatilie ili ujenzi wa jengo hilo ukamilike.

"Nilidhani hawa ndiyo wenye makosa, lakini wenye makosa ni sisi, maelekezo yangu kufikia Jumanne vifaa hivi vilinaletwa na kunipa mrejesho wa hatua mliyofikia," aliagiza Naibu Waziri Pinda.

Meneja wa TBA alimhakikishia Naibu Waziri Pinda kuwa ndani ya miezi miwili baada ya kupatiwa vifaa watakuwa wamekamilisha ujenzi wa mradi huo wa maktaba ya chuo na watafanya kazi hiyo kwa weledi mkubwa.

Mradi huo ulianza Julai 15, 2014 ukitekelezwa chini ya Kampuni ya M/S Co Ltd kwa mkataba uliotiwa saini na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ukiwa na thamani ya Sh. 2,026,538,726 (Sh. bilioni mbili).

Hata hivyo, kutokana na changamoto kadhaa ikiwamo maombi ya nyongeza ya fedha yaliyotokana na ucheleweshaji malipo kwa hati tatu za madai, ulisababisha mkataba huo kuvunjwa mnamo mwezi Juni 2021 na kutokana na umuhimu wa mradi huo tarehe 13 Juni 2022, wizara ilitia saini mikataba miwili kwa ajili ya kukamilisha mradi huo ambapo chuo kiliendelea kutekeleza ujenzi wa mkataba kwa kumtumia TBA akiwa mkandarasi mshauri.



# Wafugaji wengine waondoka kwa hiari hifadhi Ngorongoro

**Na Godfrey Mushi,** NGORONGORO

HATIMAYE kundi la 17 la jamii ya wafugaji wa kimasai limeamua kuondoka kwa hiari ndani ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), kupisha shughuli za uhifadhi.

Kundi hilo lenye kaya 47, sawa na watu 291 na mifugo 686, liliondoka juzi ndani ya hifadhi hiyo kuelekea Kijiji cha Msomera, Wilaya ya Handeni mkoani Tanga pamoja na maeneo mengine waliyochagua.

Akizungumza na Nipashe kabla ya kuondoka kwa wananchi hao, Ofisa Uhifadhi Mkuu wa NCAA, Flora Assey, ambaye ni meneja mradi wa kuhamisha wananchi wanaojiandikisha kuhama kwa hiari alisema hadi kufikia Juni 15 mwaka huu, kaya 1,519 zimeshahama Ngorongoro.

"Tangu zoezi hilo lilipoanza Juni mwaka 2022 hadi kufikia Juni 15 mwaka huu kaya 1,519 zenye watu 9,251 na mifugo 38,784 zimeshahama ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro kwenda Kijiji cha Msomera na maeneo mengine," alisema.

Aidha Assey, alifafanua kuwa kati ya kaya hizo 47, kaya 41 zenye watu 256 na mifugo 525 zimeelekea Kijiji cha Msomera na kaya sita zenye watu 35 na mifugo 161 zimeelekea maeneo mengine, ikiwamo Meatu, Simiyu na Simanjiro mkoani Manyara.

Maeneo mengine ambako wafugaji wengi wamehamia ni Saunyi na Kitwai.

Kadhalika, alisema mamlaka hiyo inaendelea na utoaji wa elimu, uhamasishaji na uandikishaji wa wananchi hao ambao kwa sasa mwitikio wa uandikishaji unaendelea kuongezeka na wananchi wengi zaidi wamefikiwa.

Awamu ya kwanza, serikali ilijenga nyumba 503 katika Kijiji cha Msomera na kuwezesha kaya 551 kuhamia zikiwa na jumla ya watu 3,010, mifugo 15,521.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (kushoto), akitoa maelekezo juzi wakati akikagua ujenzi wa Kituo cha Afya Tanzanite cha Kata ya Mirerani ambacho kinaendelea na ujenzi wake juzi. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Fakii Lulandala. **PICHA: GIFT THADEY**

# RC ashtukia 'dili' uchepushaji fedha za mradi

**Na Oscar Assenga,** MKINGA

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Buriani, ameeleza kuchukizwa kwake na kitendo cha kuchepushwa kwa fedha za mradi zilizokuwa zimepangwa kutumika kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya mama na mtoto katika Hospitali ya Wilaya ya Mkinga.

Fedha hizo pia zilipangwa kutumika katika mradi wa jengo la kuhifadhia maiti.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa Baraza Maalumu la Halmashauri ya Mkinga, lililoketi kujadili hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Dk. Buriani alisema kuwa fedha zilizochepushwa bila kibali cha ofisi yake na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni zaidi ya Sh. milioni 101.

"Nataka nipate majibu hapa, kwamba nani ametoa kibali cha fedha hizo kuhamishwa kutoka mradi mmoja kwenye mradi mwingine.

Halafu ni kwa nini fedha hizo zilipelekwa kwenye mradi mwingine, ilihali kila mradi ulipewa fedha zake," alisema.

Aliongeza: "... Kwa nini kuna idadi kubwa ya fomu za NHIF (Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya), kukakatiliwa na kurejeshwa, na siyo mwaka huu tu. Kila mwaka zinakuwa na makosa yanayojirudiarudia."

Kutokana na wilaya hiyo kukabiliwa na hoja nyingi za ukaguzi, Mkuu huyo wa Mkoa, aliagiza hoja zote kutoka kwa CAG ambazo hazijajibiwa, zijibiwe.

"Kwa mfano makusanyo kwa kutumia mashine za POS (mashine za kielektroniki), fedha ambazo hazikupelekwa benki ni zaidi ya Sh. milioni 21.97. Hilo linatokana na uzembe, hivyo lazima hatua kali ziweze kuchukuliwa," alisema.

Zaidi aliongeza: "Lakini kuna miradi yenye thamani ya Sh. milioni 107 imekamilika, lakini bado haijaanza kutumika. Sasa tunajiuliza mradi umekamilika tunakaa miezi sita, mwaka mzima tunajiuliza je, tulikuwa tunahaja na huo mradi?"

## Manyara yaibuka kidedea uchangiaji damu kitaifa

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MPANGO wa Taifa wa Damu Salama umeutangaza Mkoa wa Manyara kuwa ni kinara wa kitaifa wa kampeni ya uchangiaji damu kwa ajili ya kuokoa maisha ya wengine.

Akitangaza ushindi huo jana mjini Babati, Meneja wa mpango huo, Dk. Abdu Juma alisema Mkoa wa Manyara umechangia chupa za damu 1,512 nchini, kwamba awali ulipangiwa kukusanya chupa 1,060.

"Kama taifa, tuliamua kuja mahususi katika Mkoa wa Manyara kusherehekea miaka 20 ya uchangiaji damu. Ulikuwa ndiyo mkoa ambao ulishindwa kufikia mahitaji ya damu chupa 14,054. Mwaka 2021/2022, Manyara ilikusanya chupa 7,735, sawa na asilimia 52, na mwaka 2022/23 zilikusanywa chupa 9,260 sawa na asilimia 66," alisema.

Vilevile alisema Mkoa wa Manyara na Mkoa wa Kilimanjaro ni miongoni mwa mikoa uchangiaji wake wa damu ni mdogo, kutokana na wananchi wachache wanaojitokeza kuchangia.

Kadhalika, aliitaja sababu nyingine kuwa ni vifo vya mama wajawazito ambapo mwaka 2021 vifo vilikuwa 39 sawa na vifo 60 kati ya vizazi hai 1,000.

"Mwaka 2022 vifo 88 sawa na vifo 49 kati ya vizazi hai 1,000 na mwaka 2023 vifo 34 sawa vifo 69 kati ya vizazi hai 1,000. Eneo hili mkoa umefanya kazi kubwa kupunguza vifo," alisema Dk. Juma.

Pia alisema katika kampeni hiyo kitaifa walikusudia kukusanya chupa 40,000, hivyo aliambia umma kuwa mpaka siku ya kilele inaisha watakuwa wamezidi lengo hilo.

Katika hafla hiyo, Mkuu wa Mkoa huo, Queen Sendiga, alisema Shirika la Afya Duniani (WHO), linapendekeza kukusanya asilimia moja ya chupa za damu kwa wananchi wa nchi husika.

Sendiga aliagiza waganga wakuu wa halmashauri zote za mkoa huo kutengeneza mpango wa kukusanya damu kila halmashauri na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Awali, mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk. January Zilabumba, alisema damu ni nguzo muhimu katika kuokoa maisha na inasaidia watoto chini ya miaka mitano, wajawazito na waathirika wa ajali.

Dk. Zilabumba, alisema WHO imewezesha upatikanaji wa damu na kutengeneza sera za upatikanaji wa damu ambapo nchi 37 zilikuwa na sera hiyo mwaka 2015 mpaka kufikia zaidi ya nchi 40 zenye sera hiyo.





# Ahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kumuua mjomba

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Tabora, imemhukumu kunyongwa hadi kufa mkazi wa Wilaya ya Kaliua, Raphael Nestory pamoja na kutoa adhabu ya kifungo cha miaka minne hadi 10 jela washtakiwa wiwili, baada ya kukutwa na hatia ya kuua bila kukusudia.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu wa Mahakama ya Mkoa wa Tabora, Jovith Katto, aliyekasimishwa mamlaka ya ziada ya kusikiliza mashauri ya Mahakama Kuu, alisema Nestory, alishirikiana na wenzake kumuua mjomba wake, Elikana Lugaka, kisha kumfukia.

Katika shauri hilo, mahakama hiyo ilimwachilia huru mshtakiwa wa kwanza, Mwendapole Mayala baada ya kukosekana ushahidi wa kumtia hatiani.

Upande wa mashtaka katika kesi hiyo, ulieleza kuwa mshtakiwa (Nestory), akiwa na wenzake wawili ambao ni watoto wa marehemu Lugiko, walitenda kosa hilo Juni 4, 2020 kwa madai ya marehemu huyo alikataa kuwapatia urithi wa mali ikiwamo ng'ombe alizokuwa akimiliki.

Ulieleza kuwa watuhumiwa hao walipanga jinsi ya kumuua baba yao, walipotimiza adhima hiyo walimfukia ndani ya shimo, kisha kutokomea kusiko julikana.

Katika hatua nyingine, mahakama hiyo kwa kutumia Kifungu Namba 300 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, imebadilisha hati ya mashtaka na kumtia hatiani kwenda jela miaka minne kwa kosa dogo la kuua bila kukusudia, Twaha Shaban, aliyekuwa akikabiliwa na kesi ya mauaji.

Baada ya kusikiliza maelezo ya pande zote mbili, Hakimu Katto, alisema kwa kutumia mamlaka aliyopewa na kwa kutumia Kifungu Kidogo cha Kwanza Namba 300 anabadilisha shtaka la mauaji kuwa kosa dogo la kuua bila kukusudia.

Alisema kifungu hicho cha Sheria ya Makosa ya Jinai kinaeleza kuwa, wakati mtu anashtakiwa na kosa na maelezo yanathibitisha kwa kupunguza kosa na kuwa dogo, anaweza kutiwa hatiani kwa kosa hilo dogo japokuwa hakushtakiwa na kosa hilo.

Twaha Shaban, alikuwa anashtakiwa kwa kosa la kumuua mke wa mtoto wake, kisha kumfukia ndani ya shimo, tukio ambalo linadaiwa kutokea Januari 4 mwaka 2023 katika Kijiji cha Malanga Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora.

Vilevile, mahakama hiyo imemhukumu, Juma Ramadhan kwenda jela miaka 10 baada ya kumkuta na hatia kwa kosa la kumuua mkewe bila kukusudia.



Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude (katikati), akikata utepe kuzindua Ofisi ya Umoja wa Wazee Kata ya Masanga wilayani humo, juzi huku akiwahakikishia wazee kwamba serikali itaendelea kuwapatia huduma bora za matibabu bure na kuimarisha afya zao. **PICHA: MARCO MADUHU**

# DC atangaza operesheni kuwasaka wanafunzi watoro

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI wilayani Bukombe mkoani Geita imetangaza kiama kwa wanafunzi zaidi ya 400 wa shule za sekondari waliyoshindwa kuripoti shuleni.

Kauli hiyo imetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Bukombe, Paskasi Mragili, kueleza kuwa kati ya wanafunzi 7,532 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza walioripoti ni 6,854, huku 678 hawafahamiki walipo.

Alisema baada ya kutoa maelekezo hayo walifanikiwa kuwarejesha shuleni wanafunzi 229, kwamba kazi ya kuwasaka wanafunzi wengine 449 popote walipo inaendelea, ili warudi na kuendelea na masomo ambayo ni haki yao na waweze kutimiza ndoto zao za kupata elimu.

Alisema: "Kiwango cha ufaulu wa mtihani wa taifa ya kidato cha nne, Shule ya Bukombe Sekondari inaongoza kwa kushika nafasi ya kwanza katika Mkoa wa Geita, shida inakuja ni wazazi kutowapeleka shule watoto, licha ya serikali kuweka mazingira bora katika miundombinu ya elimu, hivyo msako huu hatokuwa na lelemama, "alisema Mragili.

Aidha, hivi karibuni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dotto Biteko, ambaye ni mbunge wa Bukombe, akiwa katika ziara yake jimboni hapo, alisikitishwa na kitendo cha watoto kutoripoti shuleni kwa sababu ya baadhi ya wazazi wanawaficha kwa makusudi.

Biteko alisema: "Wananchi wenzangu wa Bukombe Rais Samia Suluhu Hassan, anatoa fedha nyingi ili watoto wasome, tumejenga shule mpya saba za sekondari, tuna shule tano za kidato cha tano na sita, nini kinachosababisha msipeleke shule watoto? mtambue elimu katika dunia ya sasa ndiyo mlango wa maisha".

# CHADEMA yahamasisha wanachama kujiandikisha katika daftari

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Jimbo la Shinyanga Mjini, kimefanya mkutano wa hadhara na kuhamasisha wananchi wajitokeze kwa wingi kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la mpigakura.

Kazi ya kuandikisha katika daftari hilo litaanza kuboreshwa Julai, ili wapate fursa ya kupiga kura kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu mwakani.

Mkutano huo wa hadhara ulifanyika katika Uwanja wa Shule ya Msingi Town iliyopo katika Manispaa ya Shinyanga na kuhudhuliwa na viongozi mbalimbali wa chama hicho pamoja na mamia ya wananchi.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Shinyanga, Emmanuel aliwataka wananchi hao pindi uboreshaji wa daftari la kudumu la mpigakura litakapoanza wajitokeze kwa wingi kujiandikisha pamoja na daftari la makazi.

Alisema hali hiyo itawapa fursa ya kushiriki kupiga kura kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu mwakani (2025) na kupata viongozi sahihi.

Alisema: "Wananchi wa Shinyanga ili mpate viongozi sahihi wenye kupigania maslahi yenu, lazima mjitokeze kwa wingi kupigakura siku ya uchaguzi, mjiandikishe mapema kwenye daftari la kudumu la mpigakura na mkazi, ili mpate fursa ya kuchagua viongozi mnaowataka na siyo wakuchaguliwa".

Aliongeza: "Nampige kura kwa kuchagua mtu na siyo chama, kuna uongo ambao unazushwa kuwa mkichagua wapinzani hamuwezi kupata maendeleo, ni wapeni tu mfano mimi nilipokuwa Diwani wa Ngokolo mbona nilipata barabara ya lami na zile kata za CCM hakuna barabara za lami ikiwamo Kata ya Kambarage".

Mwenyekiti wa CHADEMA Jimbo la Shinyanga Mjini, Hamisi Ngunila, aliwataka wananchi wa Shinyanga wasifanye makosa, kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao utafanyika mwaka huu.

Hivyo, aliwataka wachague viongozi makini wenye uchungu na taifa, hivyo hivyo na katika Uchaguzi Mkuu mwakani.

Alisema katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwaka huu wataweka wagombea katika ngazi zote na wagombea wao ni wale ambao wapo kwa ajili ya kupigania maslahi ya jamii, kuwasomea wananchi mapato na matumizi na siyo kujali matumbo yao.

Nipashe
Spotika



CHRISTIAN ERIKSEN... UKURASA 13

# NYOTA CHIPUKIZI WA KUWATAZAMA EURO 2024

**MUNICH,** Ujerumani

Ni miaka 20 tangu Wayne Rooney kutoka England alipotangaza kipaji chake kwa ulimwengu kwenye michuano ya mataifa ya Ulaya 2004.

Nani mwingine atakuwa nyota chipukizi katika michuano ya Ulaya msimu huu wa majira ya kati ya wachezaji wote 622?

Hapa BBC Sport inawachambua wachezaji wachanga wa kutazamwa msimu huu wa majira ya joto Ujerumani.

**Martin Baturina - Croatia**

Baturina ameicheze Croatia mechi tatu hadi sasa.

Ana umri wa miaka 21. Mchezaji kiungo wa klabu ya Dinamo Zagreb na raia wa Croatia. Ni maarufu nchini kwake na amepewa jina la 'The Next Modric'!

Timu yake ni washindi wa ligi ya Crotia, na hataweza kudumu muda mrefu zaidi baada ya Euro, kwani Juventus na Arsenal zinamtaka na sio wao pekee.

**Warren Zaire-Emery - Ufaransa**

Ana umri wa miaka18, anacheza kiungo katika klabu ya PSG.

Amefanya vizuri akiwa na klabu hiyo msimu huu na kupata tuzo ya Mchezaji Bora Chipukizi wa Mwaka na mkataba mpya hadi 2029.

Benjamin Sesko - Slovenia

Ana umri wa miaka 21, ni mshambuliaji wa klabu RB Leipzig ya Ujerumani.

Sesko ni mshambuliaji mwenye mwenye futi 6 na inchi 5 ambaye mashabiki wa Arsenal wanamfahamu kwa sababu ambapo anahusishwa kutaka kujiunga nao kwa pauni milioni 50 kutoka RB Leipzig.

Aliondoka Red Bull Salzburg kwa mkopo hadi Leipzig. Aliifungia Salzburg mabao 18 msimu wa 2022-23.

**Brian Brobbey - Uholanzi**

Brobbey amepewa jina la utani 'Brobbeast' tangu siku zake za awali akiwa Ajax.

Ana umri wa miaka 22 ni mshambuliaji wa klabu ya Ajax ya Uholanzi.

Brobbey ameifunga Ajax mabao 22 katika mashindano yote. Katika kampeni ambayo wababe hao wa Uholanzi walikuwa chini kabisa ya kwenye msimamo, mchango wake uliwafikisha kufika nafasi ya tano.

Na tayari ameonja mafanikio katika ngazi ya kimataifa, akishinda mara kwa mara mashindano ya Ulaya ya Vijana chini ya miaka 17 mwaka 2018 na 2019.

**Florian Wirtz - Ujerumani**

Ana umri wa miaka 21, anachezea katika klabu ya Bayer Leverkusen ya Ujerumani.

Ni moja wa vijana wawili wa umri wa miaka 21 katika timu ya Ujerumani ambao wanajulikana sana na mashabiki wa Uingereza kutokana na ushujaa wao katika klabu.

Wirtz amekuwa mbunifu katika timu ya Leverkusen iliyotwaa ubingwa chini ya Xabi Alonso, ingawa alikosa kucheza Kombe la Dunia nchini Qatar kutokana na jeraha la goti.

Ameanza mechi saba kati ya nane tangu Julian Nagelsmann achukue usukani mwaka jana, haswa akiwa upande wa kushoto wa washambuliaji watatu.



MARTIN BATURINA

**Giorgi Mamardashvili - Georgia**

Umri wake ni miaka 23, ni kipa wa klabu ya Valencia ya nchini Hispania, anachukuliwa na wengi kuwa kipa bora kijana katika soka la Ulaya.

Mamardashvili amekuwa chaguo la kwanza kwa nchi yake, na kacheza mechi 13 za mwisho za kimashindano ya kimataifa.

**Johan Bakayoko - Ubelgiji**

Ana umri wa miaka 21, ni mshambuliaji wa kulia wa timu ya PSV Eindhoven ya Uholanzi. Alihamia PSV Eindhoven akiwa na umri wa miaka 16 kutoka Anderlecht na amefanya vyema akiwa na PSV kwa kushinda taji akiwa na mabao 16 na pasi za mwisho 14.

Majira ya joto yaliyopita ilisemekana alitakiwa na Brentford na Burnley, mwaka huu ni Bayern, Arsenal na Liverpool - inaweza kuwa vigumu kwa PSV kukataa ofa kutoka klabu hizo.

**Georgiy Sudakov - Ukraine**

Umri wake ni miaka 21, ni mchezaji kiungo wa Shakhtar Donetsk ya Ukraine.

Shakhtar Donetsk ilikataa ombi la kumuuza kwa Napoli Januari, lakini Sudakov anasema ni wakati wa kuiondoa familia yake kwenye vita na huenda akaenda London kwani amekuwa akihusishwa na klabu za Arsenal, Tottenham Hotspur na Chelsea.

**Jamal Musiala - Ujerumani**

Musiala amepewa jina la utani 'Bambi' kwa sababu ya uwezo wake wa ajabu wa kupiga chenga.

Ana umri wa miaka 21, nafasi yake ni kiungo katika klabu ya Bayern Munich ya Ujerumani.

Ndiye nyota mwingine mchanga wa Ujerumani. Inashangaza kwamba Musiala, ambaye alikulia London na kuiwakilisha Englandal kwenye timu ya taifa chini ya umri wa miaka 21, tayari yuko kwenye michuano ya tatu kwa Ujerumani.

Alianza kucheza Euro 2020 akiwa na umri wa miaka 18.

**Joao Neves - Ureno**

Umri wake ni miaka 19. Kiungo wa klabu ya Benfica. Hakukosa hata dakika moja ya msimu uliopita akiwa Benfica, alicheza kila sekunde katika michezo 12 ya Ulaya.

Alipata nafasi baada ya Enzo Fernandez alipoondoka Lisbon na kwenda Chelsea 2023. Benfica wanataka zaidi ya pauni milioni 80 kumuuza.

Ikiwa atafanya vizuri kwenye Euro 2024, kunaweza kuwa na foleni ya klabu kubisha hodi kwenye mlango wa wakala Jorge Mendes.

**Strahinja Pavlovic - Serbia**

Umri wake ni miaka 23. Ni beki wa kati wa klabu ya Red Bull Salzburg. Pavlovic amekaa kwa misimu miwili Red Bull Salzburg baada ya kusajiliwa kutoka Monaco.

Ana uwezekano wa kuanza upande wa kushoto wa safu ya kati ya wachezaji watatu wa Serbia.

**Leopold Querfeld - Austria**

Querfeld amekuwa akihusishwa kujiunga Crystal Palace, Rangers ama Celtic.

Ana umri wa miaka 20. Ni beki wa kati wa Rapid Vienna. Kwa jina la utani 'Ukuta wa Austria.'

Querfeld amekuwa beki mzuri kwa Rapid Vienna katika misimu miwili iliyopita, na alicheza mechi yake ya kwanza ya kimataifa.

**Arda Guler - Uturuki**

Umri wake ni miaka 19. Anacheza kama kiungo katika klabu ya Real Madrid.

Alijiunga na Real kutoka Fenerbahce msimu uliopita wa majira ya joto lakini akajeruhiwa vibaya, na hakucheza mchezo wowote mpaka mwishoni mwa Januari.

Akiwa na mabao sita katika mechi 12 za kwanza alizochezea akiwa na Madrid. Kocha wa Uturuki, Vincenzo Montella lazima ashawishike kumwanzisha kwenye michuano ya Ulaya.

**Xavi Simons - Uholanzi**

Umri wake ni miaka 21. Ni mshambuliaji wa PSG. Alifanya vyema akiwa kwa mkopo katika klabu ya RB Leipzig kutoka PSG msimu huu.

Alikuwa mchezaji aliyechezewa vibaya zaidi katika Bundesliga msimu huu, anapenda kuwa mtoa huduma kwa wachezaji wenzake, akimaliza nafasi ya pili kwa pasi za mwisho katika Ligi Kuu ya Ujerumani.

**Zeno Debast - Ubelgiji**

Debast amekuwa katika timu ya Anderlecht tangu 2010

Umri wake ni miaka 20. Ni beki wa Anderlecht/Sporting. Amekuwa Anderlecht tangu 2010, akijiunga na akademi hiyo akiwa na umri wa miaka sita, lakini alitangaza wiki hii: "Nimeamua kuichezea Sporting Club de Portugal msimu ujao."

Debast alikwenda kwenye Kombe la Dunia 2022 na kupata uzoefu wa mashindano, ingawa hakucheza sana.


**Mario Mitaj - Albania**

Umri wake ni miaka 20. Ni beki wa kushoto wa Lokomotiv Moscow. Baada ya mafanikio yake katika klabu ya AEK Athens, na misimu miwili yenye mafanikio sana akiwa na Lokomotiv Moscow ilifuata. Juventus wanaripotiwa kumtaka.

**Vladyslav Vanat - Ukraine**

Umri wake ni miaka 22. Ni mshambuliaji wa Dynamo Kiev. Akiwa amebarikiwa na kasi na udhibiti, Vanat alicheza mechi yake ya kwanza ya kimataifa dhidi ya Ujerumani Juni mwaka jana.

Alitia saini mkataba mpya wa miaka mitatu wa kusalia Kiev.




# VIJUE VIWANJA 10 VYA EURO

**MUNICH,** Ujerumani

UJERUMANI ni mwenyeji wa Kombe la Mataifa ya Ulaya 2024 (Euro 2024), ikiwa ni miaka 18 imepita tangu kuandaa Kombe la Dunia, ambalo Italia iliibuka mabingwa.

Fainali za Kombe la Mataifa ya Ulaya zitafanyika msimu wa majira ya joto kati ya Juni 14 na Julai 14 katika viwanja 10 katika miji 10 ya Ujerumani.

Viwanja tisa kati ya 19 vilitumika katika Kombe la Dunia la 2006, isipokuwa Dusseldorf Arena.

Ni muhimu kukumbuka kuwa jiji la Munich ni mwenyeji kwa mara ya pili mfululizo, baada ya kuwa miongoni mwa majiji 11 kuwa mwenyeji wa mashindano hayo katika msimu wa joto wa 2021.

**Olympia stadium, watazamaji 71,000**

Ni uwanja ambao mechi za timu ya Hertha Berlin (ambayo kwa sasa inashiriki ligi ya daraja la pili), ulikuwa mwenyeji wa Michezo ya Olimpiki ya 1936, fainali ya Kombe la Dunia ya 2006 na fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya 2015, na umekuwa mwenyeji wa fainali ya Kombe la Ujerumani kila mwaka tangu 1985.

Ni uwanja wenye uwezo wa kubeba watazamaji 71,000 katika jiji la Berlin, utakuwa mwenyeji wa fainali ya Kombe la mataifa ya Ulaya 2024 mnamo Julai 14.

Ulifunguliwa Agosti 1936 wakati wa utawala wa Wanazi na ukakarabatiwa 2000 na 2004 ambao kwa sasa ndio mji mkuu wa Ujerumani baada ya kuunganishwa 1990, ni moja ya miji inayovutia.

Jiji hilo linalovutia watalii, limejaa historia na utamaduni, kama vile lango la Brandenburg na mnara wa televisheni wenye urefu wa mita 368.

**Allianz Arena, watazamaji 66,000**

Uwanja huo ulijengwa na Bayern Munich na timu ya Munich 1860, ulifunguliwa mwaka 2005, kabla ya Bayern kuchukua umiliki kamili.

Ulikuwa mwenyeji wa ufunguzi wa Kombe la Dunia la 2006 na fainali ya Ligi ya Mabingwa ya 2012, wakati Chelsea ilipowafunga wenyeji Bayern Munich kwa mikwaju ya penalti.

Pia mechi za Kombe la Ulaya la 2020 katika msimu wa joto wa 2021 zilichezwa.

Ndio uwanja wa mechi ya ufunguzi kati ya Ujerumani na Scotland Juni 14 na moja ya mechi mbili za nusu fainali.

Munich ni nyumbani kwa watu milioni 1.6. Ni jiji la tatu kwa ukubwa nchini Ujerumani, eneo lililojaa historia, majumba, bustani na kitovu cha unywaji bia.

**Signal Iduna Park, watazamaji 62,000**

Uwanja wa timu ya Borussia Dortmund ni mojawapo ya viwanja maarufu duniani kutokana na ukuta wa njano wa mashabiki. Ulifunguliwa mwaka 1974 na ukafanyiwa ukarabati 2003.

Umetumika kwenye mechi muhimu, ikiwa ni pamoja na Fainali ya Kombe la UEFA ya 2001 kati ya Liverpool na Alaves ya Hispania.

Utatumika kucheza moja ya mechi mbili za nusu fainali katika Kombe la Ulaya la 2024.

Dortmund ni kitovu cha utamaduni wa eneo la Ruhr. Eneo hilo lilikuwa maarufu miaka 50 iliyopita kwa makaa ya mawe, chuma na bia, lakini kwa sasa ni maarufu kwa teknolojia.

**MHP Arena, watazamaji 51,000**

Uwanja huo umekarabatiwa na kuwa wa kisasa zaidi tangu kujengwa kwake 1933. Ulitumika katika Kombe la Dunia la 1974 na 2006, Kombe la Ulaya la 1988 na fainali ya Kombe la Ligi ya Mabingwa 1959 na 1988, pamoja na Riadha ya Dunia ya 1993.

Upo katika mji wa Stuttgart, ni mojawapo ya miji muhimu ya viwanda na makao makuu ya watengenezaji magari Mercedes na Porsche.

**Volkspark stadium, watazamaji 49,000**

Uwanja huo ulifunguliwa kwa mara ya kwanza mwaka1953, ukafanyiwa ukarabati mwaka 2000, na kuandaa mechi za Kombe la Ulaya la 1988 na Kombe la Dunia la 1974 na 2006.

Volksparkstadion upo katika mji wa Hamburg, mji wenye bandari kubwa ya kimataifa, historia tajiri ya kitamaduni, usanifu mzuri majengo na maisha ya usiku ambayo huwa kivutio kwa watalii wengi.

**Mercur Spiel Arena, watazamaji 47,000**

Unamilikiwa na timu ya Fortuna Düsseldorf, ambayo ilishiriki mara ya mwisho ligi kuu katika msimu wa 2019/2020.

Uwanja huo, ambao zamani ulijulikana kama Reheinstaedon, ulikuwa mwenyeji wa mechi za hatua ya makundi za Kombe la Ulaya la 1988.

Dusseldorf, mji mkuu wa jimbo la Rhine-Westphalia Kaskazini, mji huo una wakazi 650,000. Rhine-Westphalia ni jimbo lenye watu wengi zaidi nchini Ujerumani.

Rhein Energie Stadium, watazamaji 43,000

Uwanja wa klabu ya Cologne, ilishuka daraja hadi daraja la pili, ulikarabatiwa kwa ajili ya maandalizi ya Kombe la Dunia 2006, baada ya kufunguliwa mwaka 1923 na kufanyiwa ukarabati wa awamu ya kwanza mwaka 1975.

Ulikuwa mwenyeji wa mechi za Kombe la Ulaya 1988, Kombe la Shirikisho 2005 na Kombe la Dunia la 2006.

Tangu 2010, hutumika kwa fainali ya Kombe la Wanawake la Ujerumani, pamoja na mechi za mpira wa magongo na matamasha.

Cologne nyumbani kwa zaidi ya watu milioni moja. Ni nyumbani kwa maeneo muhimu zaidi ya watalii nchini Ujerumani kama Kanisa Kuu la St. Peter, urithi wa dunia wa UNESCO.

**Deutsche Bank Park, watazamaji 47,000**

Uwanja wa timu ya Eintracht Frankfurt ulifunguliwa Mei 1925. Ulikuwa mwenyeji wa mechi za Kombe la Dunia la 1974, ikijumuisha ufunguzi, Kombe la Ulaya la 1988, Kombe la Shirikisho la 2005 na Kombe la Dunia la 2006.

Frankfurt ni eneo la kimataifa la fedha na biashara, mji huo uko kwenye kingo za mto Main. Ni jiji la tano kwa ukubwa nchini Ujerumani na maghorofa yake ya kipekee limepewa jina la utani "Manhattan."

**Red Bull, watazamaji 40,000**

Ni uwanja wa kisasa wenye paa la kisasa ambalo lilifunguliwa mwaka 2004. Ni uwanja pekee utakao chezewa kombe la Ulaya katika eneo la iliyokuwa Ujerumani Mashariki.

Ulitumika katika mechi za Kombe la Dunia la 2006. Ni uwanja wa klabu mpya ya RB Leipzig tangu 2010.

Mji wa Leipzig umejaa historia na ndipo alipoishi mwanamuziki Johann Bach siku za nyuma. Mji huo ulishuhudia maandamano ya amani mwaka 1989 huku Ujerumani ikijiandaa kuunganisha sehemu hizo mbili.

**Veltins, watazamaji 50,000**

Uwanja huo ulifunguliwa mwaka 2001 na ni nyumbani kwa timu ya Schalke FC, bingwa mara saba wa Ujerumani na kwa sasa inashiriki ligi ya daraja la pili.

Una paa linaloweza kufunguliwa na kufungwa. Uwanja huo uliandaa fainali ya Ligi ya Mabingwa ya 2004 na robo fainali ya Kombe la Dunia la 2006.

Upo katika jiji la Gelsenkirchen, lililokuwa maarufu kwa makaa ya mawe na chuma, lakini siku hizi ni kijani kibichi, sinema, safari za boti, na viwanda vya kale.

## Nukuu

"Najaribu kuandaa timu katika namna bora, na tunaangalia ni namna gani tunaweza kuanza vizuri kwenye haya mashindano," **Kocha wa timu ya taifa ya England, Southgate akizungumzia timu yake kwenye mashindano ya Euro 2024.**



"Ni mtu ambaye ana aina yake ya falsafa ambayo sisi kama Brighton & Hove Albion tunataka icheze, nina uhakika ni mtu atakayetusaidia," **Mwenyekiti wa Klabu ya Brighton, Tony Bloom.**



"Sio kitu ninachokifikiria, kwa sasa naangalia zaidi mambo ya mbele, kuendelea kucheza soka na kuwa sahihi kwenye mpira" **alisema kiungo wa Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen.**





Abdelhak Benchikha, raia wa Algeria, ni mmoja wa makocha 18 waliotimuliwa hadi kumalizika kwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu 2023/24, akiwa anaifundisha Simba.

# LIGI KUU ILIVYOONDOKA NA 'VICHWA' VYA MAKOCHA 18

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara msimu wa 2023/24, ilioanza kutimua vumbi, Agosti 15 mwaka jana na kutamatika, Mei 28, ilisababisha makocha 18 kutimuliwa au kujiuzulu kwa sababu mbalimbali, ikiwamo kufanya vibaya kwa timu zao.

Kwa mujibu wa rekodi za dawati letu la michezo, Singida Fountain Gate, ndiyo timu iliyoongoza kwa kutimua makocha wengi kuliko timu zote, huku timu tano tu kati ya 16, ndizo zilizoanza na kumaliza msimu wa makocha wao.

Jumla ya makocha 13 wazawa ndiyo waliopata nafasi ya kufundisha timu za Ligi Kuu msimu uliomalizika 2023/24.

Mwandishi wa makala haya anakuletea taarifa za timu zote 16 zilizocheza Ligi Kuu na idadi ya makocha waliowatumia, huku akiorodhesha wote 19 ambao waliondoka kwenye vikosi vyao kabla ya kumalizika.

**1. Yanga**

Ndiyo timu iliyochukua ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu kwa kukusanya pointi 80.

Kiwango chake, ushindi iliyokuwa inaupata, wala haikushangaza kubaki kwa kocha wake yule yule, raia wa Argentina, Miguel Gamondi.

**2. Azam FC**

Licha ya kukamata nafasi ya pili kwa pointi 69, lakini ikiendelea kuwa kocha wake yule yule inayomtambua kama Kocha Mkuu, Msenegal, Youssouph Dabo, mwanzo wa ligi hadi mwisho.

**3. Simba**

Imeshika nafasi ya tatu hadi kumalizika kwa Ligi Kuu msimu uliomalizika. Mpaka inamaliza ligi tayari ilikuwa imeshaondokewa na makocha wawili. Ilianza na Roberto Oliveira raia wa Brazil, lakini alitimuliwa baada ya kipigo cha fedheha cha mabao 5-1 ilichokipata dhidi ya watani wao wa jadi, Yanga, Novemba 5 mwaka jana.

Jahazi likachukuliwa na kocha raia wa Algeria, Abdelhak Benchikha. Hata hivyo naye kabla ya mechi chache tu kukamilika kwa ligi, 'rigwaride' likamshinda, akabwaga manyanga mwenyewe, baada ya kuona jahazi linakwenda mrama, Kocha Mtanzania, Juma Mgunda ndiye alichukua jukumu la kumalizia ligi.

**4. Coastal Union**

Nafasi ya nne haikupatikana kwa lelemama, ilibidi viongozi wa timu hiyo kumtimua kocha, Mwinyi Zahera, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo. Wakati wanamtimua walikuwa chini kwenye msimamo msimamo wa Ligi Kuu, wakati wa mzunguko wa kwanza.

Ikaamua kumleta Mkenya, David Ouma. Ikabaki historia. Leo hii imekata tiketi ya kucheza Kombe la Shirikisho Afrika.

**5. KMC**

KMC ni timu moja kati ya timu tano ambazo zilianza na kocha wao mkuu na kumaliza naye Ligi Kuu msimu uliomalizika. Ilianza na Abdulhamid Moalin, raia wa Somalia, ambaye ameifanya timu hiyo kumaliza nafasi ya tano.

**6. Namungo FC**

Mpaka inamaliza ligi, ikikamata nafasi ya sita, tayari ilikuwa imetimua makocha wawili. Wa kwanza ni Mrundi Cedric Kaze aliyewahi kuifundisha Yanga, akaja Denis Kitambi ambaye awali alikuwa msaidizi, naye baadaye akaonyeshwa mlango wa kutokea, mwishoni wakamchukua Zahera akitokea Coastal Union, akamalizia ligi.

**7. Ihefu FC**

Timu hii ambayo kwa sasa inaitwa Singida Black Stars, ikihama kutoka Mbarali, Mbeya na kwenda kufanya maskani wake mkoani Singida, ilianza na kocha Zubari Katwila. Hata hivyo katikati ya msimu aliondolewa na nafasi yake ikachukuliwa na Mecky Maxime, aliyemaliza msimu, akaifikisha nafasi ya saba.

**8. Mashujaa FC**

Timu ya Mashujaa inaunda mtandao wa timu tano ambazo hazikuwagusa makocha wake msimu huu. Ilianza na Mohamed Abdallah 'Bares' na ikamaliza naye, japo ilianza kwa kusuasua muda mrefu wa ligi, lakini ikamaliza kwa kishindo ikiwa nafasi ya nane.

**9. Prisons**

Hadi msimu wa kwanza unamalizika, ilikuwa moja kati ya timu zilizokuwa hoi bin taaban, zikitabiriwa kushuka msimu uliomalizika. Ilichofanya, pamoja na usajili wa dirisha dogo, ikimtimua kocha wake, Fred Felix Minziro na kutwaa, Ahmad Ally. Ni kocha aliyefanya kazi kubwa na imeonyesha kwa kuimalika ikiwa kwa timu katika msimamo wa Ligi Kuu iliyomalizika.

**10. Kagera Sugar**

Hapa kulikuwa kama kuna mabadilishano ya makocha tu. Baada ya kuona mambo yanakwenda mrama, Kagera Sugar ikaachana na Maxime, ikamchukua Minziro ambaye alikuwa ameoshwa mlango wa kutokea na Prison.

Wakati Mexime akienda Ihefu, Minziro alimaliza msimu akiwa na timu hiyo, akiwezesha kumaliza nafasi ya 10.

**11. Singida Fountain Gate**

Hii ndiyo timu iliyotia fora ya kutimua makocha wengi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2023/25. Imetimu makocha watano tofauti kwa sababu mbalimbali, ikiwamo kufanya vibaya.

Ilianza na Mholanzi, Hans van Pluijim, ikamtimua, akaja Mjerumani, Ernst Middendorp ambaye hakukaa hata mwezi, kaingia Mbrazil Ricardo Heron Ferreira, naye pia hakukaa sana, kocha msaidizi Msauzi, Thabo Senong akashika usukani. Wala haikusaidia, naye akatimuliwa, Jamhuri Kihwelo akashika hatamu, yakamshinda, mwishoni akamalizia Ngawina Ngawina.

**12. Dodoma Jiji**

Ilimaliza nafasi ya 12, yenyewe ilitimua kocha mmoja, Melis Medo, ikamtwaa Mkenya, Francis Baraza ambaye alichukuwa jukumu hilo hadi mwisho.

**13. JKT Tanzania**

Timu hii inakamilisha timu tano ambazo hazikutimua kocha yoyote tangu mwanzo mwa ligi, ikiwamo Yanga, Azam, KMC na Mashujaa FC. Ilikuwa na Malale Hamsini, mwanzo hadi mwisho wa ligi.

**14. Tabora United**

Ilianza na kocha wa zamani wa Simba, Goran Kopunovic, lakini ikaachana naye, ikamtwaa, Mfaransa, Lauren Goevec, akawa mmoja wa makocha waliokaa muda mfupi zaidi, akaja Masoud Djuma akamalizia ligi, ikienda kwenye 'play off'. Hata hivyo ametimuliwa baada ya ligi kumalizika na hakwenda kwenye 'paly off', hivyo anahesabika kama alimaliza nayo kwani hakutimuliwa kabla kama wengine.

**15. Geita Gold**

Awali ilikuwa na Hemed Morocco, lakini baadaye hawakuelewana, akaondoka na kulewa Denis Kitambi ambaye alikuwa ametimuliwa kutoka Namungo. Matokeo ya yote ikashuka daraja.

**16. Mtibwa Sugar**

Habib Kondo ndiye aliyeanza nayo ligi, lakini chombo kilipoonekana kwenda mrama, akachukuliwa Katwila ambaye alikuwa ametimuliwa Ihefu. Haikuwa dawa, tangu awali ilionekana kama itashuka daraja na kweli ikawa hivyo.

**JE, WAJUA?**




Golikipa wa klabu ya Millwall, Matija Sarkic, amefariki dunia hivi karibuni akiwa na miaka 26. Golikipa huyo wa kimataifa wa Montenegro alijiunga na klabu hiyo ya 'Championship' akitokea klabu ya Wolves mwaka 2023 na kucheza michezo 33 msimu uliopita.



# TIC yaingia mikataba uzalishaji sukari, soya, mahindi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimesaini mikataba ya makubaliano ya kukodisha mashamba ya Mkulazi mkoani Morogoro, hekta 30,000 kwa kampuni tatu.

Mikataba hiyo italenga uzalishaji sukari, soya na mahindi ya njano wenye uwekezaji wa zaidi ya Sh. trilioni 1.2.

Mkurungezi Mtendaji wa TIC, Gilead Teri, alisema hayo juzi jijini hapa, baada ya hafla ya utiaji saini mikataba hiyo iliyoshuhudiwa na Waziri wa Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe pamoja na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe.

Teri, alisema utiaji saini wa mikataba hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa Jiji la kilimo Mkulazi ambapo kampuni hizo zitafanya uwekezaji mkubwa katika kilimo cha miwa kwa ajili ya uzalishaji sukari na kilimo cha soya na mahindi ya njano kwa ajili ya kuuza nje.

Alisema, katika hekta hizo 30,000 za mashamba kila kampuni itapata hekta 10,000 kwa ajili ya kilimo na kiasi ambacho kinatakiwa kutumia katika uwekezaji huo ni zaidi ya Sh. trilioni 1.2.

Alizitaja kampuni hizo kuwa ni Long Pin pamoja ya Tanzania pamoja na Eagle Hills na Food Platform, kutoka China na India.

Aidha, alisema uwekezaji huo unatarajiwa kutoa ajira za moja kwa moja 9,000 na zisizokuwa za moja kwa moja 11,000.

Akizungumza katika hafla hiyo, Prof. Mkumbo, aliipongeza TIC, kwa kusaini mkataba huo wenye uwekezaji mkubwa nchini akisema utakwenda kusaidia uzalishaji wa sukari pamoja na uuzaji wa mahindi ya njano na soya nje ya nchi.



Mtendaji Mkuu wa Asasi isiyo ya Kiserikali ya Water Gate Community Link, John Mudende, akifurahia juzi na wanafunzi wa Shule ya Msingi Migilango wilayani Iramba mkoani Singida baada ya kuzindua mradi wa maji katika kijiji hicho ambao umejengwa kwa ufadhili wa Poul Due Jensen Grundfos Foundation ya nchini Denmark kupitia asasi hiyo. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Serikali kukabiliana usugu wa vimelea vya magonjwa

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema serikali inafanya jitihada za kukabiliana na Usugu wa Vimelea vya Magonjwa Dhidi ya Dawa (Uvida).

Alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki mkoani Dodoma alipofanya mazungumzo na balozi wa kampeni ya Holela-Holela itakukosti, Kido ambayo inasisitiza mbinu kamilifu ya 'afya moja' kushughulikia tatizo la Uvida na magonjwa ambayo yanaweza kuambukizwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa wanadamu.

Alisema Uvida bado ni tatizo kubwa nchini na athari zake ni kama vile ugonjwa kujirudia mara kwa mara na kuchukua muda mrefu kupona.

Alitaja athari zingine ni kuenea na kusambaa kwa vimelea sugu vya magonjwa dhidi ya dawa, ulemavu na hata kifo.

"Mbali na hapo kuna athari za kiuchumi kama vile kutumia gharama kubwa kwenye matibabu, hivyo kupungua kwa pato binafsi, la familia na taifa," alisema Ummy.

Pamoja na mambo mengine, Ummy alisisitiza juu ya Uvida na magonjwa yanayoambukizwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu ambayo kampeini ya Holela-Holela Itakukosti imelenga.

"Naomba nichukue fursa hii nitoe wito kwa jamii kuwa Mtanzania anaweza kufanya mambo machache tu kukabiliana na Uvida kama vile kupata na kufuata ushauri wa mtaalamu wa afya kabla ya kutumia dawa, kutumia dozi ya dawa kikamilifu," alisema.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa USAID Tanzania, Alex Klaits, alisema: "Kampeni inaonyesha jukumu muhimu la ushirikiano katika kuleta athari chanya na kuhakikisha uendelevu wa muda mrefu, ikiwaleta pamoja wadau wa afya kutoka sekta mbalimbali kupambana na Uvida."

Kampeni hiyo ilizinduliwa mwezi uliopita kwa uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana Wizara ya Afya, Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Wizara ya Mazingira, ikifadhiliwa na USAID kupitia mradi wa Breakthrough action.

# Wananchi 141,521 kuandikishwa daftari wapigakura Iramba

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

WANANCHI 141,521 wanatarajia kuandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwaka huu katika Wilaya ya Iramba mkoani Singida.

Ofisa Uchaguzi Wilaya ya Iramba, Elia Ziwa, alisema hayo juzi wakati wa kutoa elimu kwa viongozi na wananchi wa kata za Mgongo, Ntwike na Tulya kuhusu umuhimu wa kujiandikisha katika daftari hilo.

Alisema idadi hiyo wanaotarajia kuandikishwa mwaka huu ni ongezeko la watu 9, 985 ya watu 131,536 waliolengwa kuandikishwa mwaka 2019 ambapo hadi zoezi hilo linafungwa waliandikishwa watu 98,000.

Ziwa alisema kuwa kuna umuhimu wa kila mtu kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura ili kupata taarifa zake kwenye vitongoji, vijiji na kata, hali itakayompa fursa ya kushiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu.

Aidha, aliwakumbusha viongozi na wananchi kuwa utaratibu wa huko nyuma wa mtu kupita bila kupingwa hautakuwapo tena katika uchaguzi wa mwaka huu na wa mwakani, badala yake hata mgombea awe wa chama kimoja ama yupo peke yake ni lazima kura zipigwe.

Ofisa Uchunguzi kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wilayani Iramba, Michael Ngomo, alisema kuwa taasisi hiyo imejipanga kuhakikisha inazuia vitendo vya rushwa wakati wa chaguzi zote.

# Wadau wakoshwa uandaaji kanuni Uchaguzi S/Mitaa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WADAU wa uchaguzi nchini wamesema hatua ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuandaa kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni sahihi na haivunji sheria yoyote.

Akichangia juzi jijini hapa, kwenye kikao cha utoaji maoni kuhusu Rasimu ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Mkurugenzi Mtendaji wa shirika lisilo la kiserikali la Women in Social Entrepreneurship (WISE), Dk. Astronaut Bagile, alisema wananchi wanapaswa kuelewa kuwa hakuna sheria yoyote imevunjwa katika mchakato wa uchaguzi huo.

Dk. Bagile alisema ukatili wa kijinsia umekuwa kikwazo kwa wanawake kushiriki kwenye uchaguzi na kusisitiza kuwa kanuni hizo zinaenda kuwabana wale wote wanatoa kejeli matusi na vitisho kwa wanawake ambao wanajitokeza kuwania nafasi za uongozi.

Akifungua kikoa hicho, Naibu Waziri TAMISEMI, Dk. Festo Dugange, alisema Sheria ya Serikali za Mitaa inampa dhamana waziri mwenye mamlaka za serikali za mitaa kuandaa Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kusimamia.

Dk. Dugange alisema maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kutaka Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka huu kuwa huru na haki na kwamba rasimu hiyo imezingatia maoni ya wadau.

Shekhe Mkuu wa Jumuiya ya Shiha (TIC) Tanzania, Hemed Jalala, alipongeza hatua ya serikali ya kuwashirikisha viongozi wa dini na watu wengineo katika kutoa maoni.

Alisema hatua ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI kuwakutanisha viongozi wa dini kutoka maeneo tofauti ni ishara ya nia njema ya Rais Samia ya kutenda haki na kuimarisha demokrasia nchini.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Elim Pentekoste Tanzania, Peter Konki, aliishauri serikali kuongeza wigo wa kupokea maoni kuhusu maboresho ya rasimu ya kanuni hizo.

Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Charles Kitima, alishauri kuwepo uwazi wakati wa wagombea wanaporejesha fomu ili kuondoa manung'uniko pale mtu anapoenguliwa kushiriki uchaguzi.





# Msako waja nyumba kwa nyumba wachafuzi pareto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeunda kikosi kazi maalum kufanya ukaguzi nyumba kwa nyumba kuwasaka wakulima wanaouza maua ya pareto ambayo hayana ubora ili kunusuru kuporomoka kwa zao hilo katika soko la dunia.

Tanzania ni nchi ya pili duniani na ya kwanza Afrika kwa kulima zao hilo hivi karibuni inahofia kuporomoka kwenye nafasi hizo kutokana na baadhi ya wakulima kuuza maua ambayo hayajakidhi ubora.

Akizungumza kwenye mafunzo ya mawakala wa zao hilo yaliyotolewa na kampuni ya PCT katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, mwakilishi wa Bodi ya Pareto nchini Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Edwin Margwe, alisema kikosi hicho kitakuwa kinafuatilia ubora wa maua hayo kuanzia shambani hadi kwenye vituo vya mawakala.

Margwe, alisema kampuni zote ya pareto zilikubaliana kwenye kikao maalum na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa kutonunua maua hayo ambayo hayana ubora na atakayebainika ameuza au kununua hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Alisema kikosi hicho, kitahusisha vyombo vya usalama, maofisa wa Wizara ya Kilimo, halmashauri, kampuni na ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

Aliwataka mawakala kuacha kupokea maua yaliyoanikwa chini kwa kuwa ndio chanzo cha kupoteza ubora wa zao hilo na kuporomoka katika soko hilo la dunia.

Alisema maua hayo yanatakiwa kuanikwa kwenye turubai, kwamba mawakala hawatakiwi kununua pareto kutoka kwa wakulima ikiwa bado haijakauka na kuchumwa maua hayajakomaa.

Ofisa Pareto Mkoa wa Songwe na Mbeya (PCT), Musa Malubalo, alisema tatizo la maua yasiyokuwa na ubora inazisababishia hasara kampuni za pareto kwa kuwa sehemu kubwa haifai kupelekwa sokoni, inakuwa ni takataka.

Malubalo alisema katika msimu wa kilimo uliopita, PCT ilipata hasara ya zaidi ya Sh. bilioni moja kwa kuuziwa maua machanga na kutofikia kiwango kinachowezesha kuzalisha sumu kiwandani.

Alisema hakuna kampuni iko tayari kununua maua ambayo hayana ubora kwenye soko la ndani na nje ya nchi.

Baadhi ya mawakala walisema ushindani wa kampuni, tamaa ya fedha na baadhi ya mawakala kutokuwa waaminifu vinasababisha baadhi yao kununua maua yasiyokuwa na ubora.



Meneja Huduma za Utangazaji wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mhandisi Andrew Kisaka, akitoa elimu kwa waandishi wa habari kuhusu wajibu na majukumu ya vyombo vya habari katika kuelimisha umma wakati wa semina ya siku mbili ya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura iliyoandaliwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wafugaji waomba kupatiwa mitamba

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAFUGAJI jamii ya wamasai wanaomiliki ranchi ya Matebete iliyoko wilayani hapa Mkoa wa Mbeya, wameiomba serikali kutoa elimu ya ufugaji wa kisasa na kuwapatia madume bora ya ng'ombe (mitamba) ili waanze kupata tija.

Walitoa ombi hilo kupitia risala yao iliyosomwa mbele ya Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Taifa, Mrida Marocha baada ya kutembelea ranchi hiyo, kusikiliza kero za wafugaji.

Katibu wa wafugaji wa ranchi hiyo, Matei Kurubai, alisema hawana elimu na mbinu za kufuga kisasa na hawafahamu namna ya kupata pembejeo kwa ajili ya mifugo.

Katibu wa Chama cha Wafugaji Taifa, Mathayo Mgusa, aliwaomba wataalamu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kufika kwenye ranchi hiyo kutoa elimu ili iwe mfano kwa ranchi nyingine nchini.

Mwakilishi kutoka Wizara ya Mifugo, Emmanuel Augustine, aliwataka wafugaji hao kuhakikisha wana maji ya kutosha kwa ajili ya mifugo na kupata ng'ombe wa kisasa ili kuongeza tija.

Augustine alisema serikali inaendelea kuboresha sekta ya ufugaji ili iwe sehemu ya sekta zinazochangia kwa kiwango cha ukuaji wa pato la taifa na kuwainua wafugaji.

Alisema mazao ya mifugo yamekuwa yakisafirishwa kwenda kuuzwa nje ya nchi ikiwamo ngozi na nyama na kwamba serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya usafirishaji.

Akizungumza baada ya kupokea risala hiyo, Marocha alitoa rai kwa wafugaji wa ranchi hiyo kulinda eneo hilo ili kuhakikisha linatumika ipasavyo kwa shughuli za ufugaji kwa faida ya wafugaji wenyewe na taifa.

Hivyo, aliwataka wafugaji wa maeneo mengine kuiga mfano wa wafugaji hao akisema kunapunguza migogoro ya ardhi kati yao na wakulima.

Pia, aliwataka wafugaji wa Wilaya ya Mbarali kuacha kuingiza mifugo kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha hasa Bonde la Ihefu ili kupunguza hasara kutokana na mifugo yao kutaifishwa.

# Wakulima kunufaika msaada mbegu, miche, vikaushio

**Na Elizabeth John,** MAKETE

WAKULIMA walio chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) mwaka 2024/25 wilayani Makete Mkoa wa Njombe wanatarajia kunufaika na msaada wa mbegu, miche na vikaushio kutoka Kampuni ya Pareto Tanzania (PCT) ili kujikwamua na umaskini.

Akizungumza katika mkutano wa wadau wa pareto, Mwakilishi wa PCT, Gerald Joseph, alisema wameanzisha mkakati mahususi wa kukomboa kaya maskini kupitia kilimo.

Alisema pia wanahudumia wakulima walio nje ya vikundi takribani 3,865 ambapo kwa kupindi cha kuanzia mwaka 2019 hadi Machi 2024 wameilipa Makete Sh. milioni 41.3 kama ushuru wa zao hilo.

Joseph alisema ili kupata pareto bora ni lazima kuzingatia kanuni bora za kilimo kwa wadau waliopo katika mnyonyoro wa uzalishaji ambao ni wakulima, mawakala, wanunuzi na serikali.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alisema kupitia kilimo hicho ana mararajio ya kuona wakulima wananufaika kiuchumi kupitia ardhi waliyobarikiwa na Mungu.

"Ardhi ya Makete ni nzuri ina mvua misimu miwili kwa mwaka na hata ukipanda kidole kinaota, hii sio wilaya maskini na kwenye vikao vyangu sipendi kujadili umaskini," alisema Mtaka.

Alisema mpango uliopo ni kuhakikisha kunajengwa taswira na kufuta umaskini kuanzia ngazi ya familia.

Mwenyekiti wa wakulima wa pareto Tanzania, Anangisye Mwankina, alisema pamoja na kuhamasisha kilimo hicho, kampuni za ununuzi zifanye utaratibu wa kutoa mikataba ili kiwe na tija.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete, William Makufwe, alisema pareto ni moja ya zao la kimkakati katika halmashauri yao.

# Wakulima mpunga wapewa elimu matumizi teknolojia

**Na Gwamaka Alipipi**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imewakutanisha wakulima wa mpunga kutoka mikoa ya Pwani, Tanga na Mbeya, lengo likiwa ni kuwawezesha kufanya kilimo chenye tija kwa kutumia teknolojia za kisasa.

Pia, mafunzo hayo yalilenga kuwawezesha wakulima hao kuachana na kilimo cha mazoea, pamoja na kuwapatia mikopo itakayowawezesha kuongeza mitaji katika kilimo chao.

Akizungumza na waandishi wa habari Ofisa Biashara Mwandamizi TADB, Angelina Nyansambo, alisema wakulima waliokutana katika mafunzo hayo ni kutoka Chama cha Ushirika wa Wakulima wa Umwagiliaji Ruvu (CHAURU) na Chama cha Ushirika wa Wakulima Umwagiliaji Mombo.

Alisema pamoja na mambo mengine wakulima hao walitembelea kiwanda cha kukoboa mchele cha Raphael Group Company Limited, Azimio Uswisi na kukutana na wakulima wa Chama cha Umwagiliaji Mbuyuni mkoani Mbeya.



## Waziri ataja faida uchangiaji damu kwa hiari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma amesema uchangiaji damu ni miongoni mwa mambo muhimu yanayopaswa kupewa kipaumbele.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa maadhimisho ya Siku ya Uchangiaji Damu Salama Duniani, yaliyofanyika Mjini Unguja.

Alisema hali ya uchangiaji damu haifungamani na mfumo wowote wa kijamii kama kisiasa, kidini, wala kikabila.

Alisema lengo la maadhimisho ya siku hiyo ni kuwashukuru, kuwapongeza, kuwajali na kuendelea kuwahamasisha wachangiaji damu na watu wengine ambao wanaweza kujitolea ili kuokoa maisha ya wengine.

Alisema suala la kuchangia damu ni jambo la kibinadamu linalomgusa kila mtu na ndiyo maana katika hafla hiyo kuna mkusanyiko wa makundi mbalimbali wakiwemo walimu na wanafunzi wa shule, vyuo, wananchi wa kawaida, viongozi wa dini na vikosi vya ulinzi na usalama.

Alisema asilimia kubwa ya watumiaji wa damu ni wajawazito hasa pale wanapopoteza damu nyingi wakati wa kujifungua, watoto chini ya umri wa miaka mitano, waathirika wa ajali na upasuaji unaohitaji kutumia tiba ya damu.

Alisema juhudi za kuelimisha jamii zaidi huhitajika katika shuguli hizo na wananchi waliowengi wanayo elimu ya wastani juu ya kuchangia damu kwa hiari.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Habiba Omar Hassan alisema zoezi la uchangiaji wa damu Zanzibar lilianza mwaka 2005 na ilianza kwa dharura.

Alisema hakuna tiba mbadala wa damu, hivyo ni lazima mhitaji achangiwe ili kusaidia kuokoa maisha ya wengine.

Akisoma risala ya wachangiaji wa damu, Fatma Rashid alisema pamoja na kuadhimisha siku hiyo lakini pia ni kusherehekea kutumia kwa miaka 20 ya uchangiaji wa damu duniani.

Hata hivyo alisema kwa upande wa Zanzibar wachangiaji wa damu wanakabiliwa changamoto mbalimbali zikiwemo kutothaminika hospitali wakati wa kuhitaji kuitumia huduma hiyo kwa wagonjwa wao.

Alitaja changamoto nyingine ni kupokea kauli zisizoridhisha kwa baadhi ya wahudumu wa afya pamoja na kutoviendeleza vikundi vya wachangiaji damu na makundi malumu.

# Serikali kusimamia malengo ya kigoda cha Hayati Karume

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema serikali itahakikisha inafanikisha malengo mahususi ya kuanzishwa kwa kigoda cha taaluma ya ukombozi na maendeleo ya Afrika cha Hayati Abeid Amani Karume.

Amesema lengo ni kuleta tija za kihistoria, kitaaluma na maendeleo kwa ustawi wa Zanzibar. Aliyasema hayo wakati wa ufunguzi wa kigoda hicho katika ukumbi wa Dk. Ali Muhammed Shein, Tunguu Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja.

Dk. Mwingi alisema serikali inatambua majukwaa kama hayo yapo mengi kwenye mataifa mengi duniani na kwa majina tafauti, ambayo yamesaidia kufanikisha masuala ya kitaaluma na maendeleo kupitia fani mbalimbali kwa utafiti, mijadala, maandiko na mapendekezo kwa serikali. Hivyo, alizitaka taasisi binafsi na mashirika mengine ya ndani na ya kimataifa kushirikiana na serikali katika kukisaidia kigoda hicho kiendelee kutekeleza majukumu yake. Alisema Hayati Abeid Amani Karume alikuwa kiongozi shujaa, mzalendo aliyejitolea kuleta uhuru na maendeleo ya Zanzibar na Afrika baada ya kuongoza Mapinduzi ya Zanzibar yaliyoleta uhuru wa kisiasa, kiuchumi na kijamii. Akitaja malengo ya kigoda hicho Dk. Mwinyi alisema ni pamoja na kuhifadhi, kuibua na kueneza mawazo na fikra za Hayati Abeid Amani Karume kupitia utafiti, mijadala, makongamano, mikutano na machapisho mbalimbali. Alisema pia kuendeleza ushirikiano wa ndani na nje ya Afrika uliouanzisha baada ya mapinduzi.

Kadhalika, aliwasihi wanataaluma kutumia fursa ya kufanya utafiti na kazi nyingine za kitaaluma kupitia kigoda hicho ili kustawisha taaluma zao na kuleta mchango kwa Wazanzibar. Akichangia mada ya mchango wa Hayati Abeid Aman Karume katika siasa za Zanzibar, Tanzania na Afrika, Rais Mstaafu Jakaya Kikwete alipongeza fikra, busara na maono ya Hayati Karume kwenye ukombozi wa Zanzibar dhidi ya ukoloni na utumwa. Pia aliwataka Watanzania kuzitumia fursa za maendeleo zilizopo baina ya pande mbili za muungano sambamba na kuzitunza, kuzilea, kuziimarisha fikra za mapinduzi na muungano.

Alisema kuanzishwa kwa kigoda hicho siyo heshima kwa Zanzibar pekee lakini kwa Tanzania na tasnia yote ya elimu nchini.

Balozi wa kigoda hicho, Rais Mstaafu wa Zanzibar, Dk. Aman Abeid Karume alipongeza serikali kwa wazo la kuanzishwa kwa kigoda hicho ili kuzienzi, kuzitunza na kuziendeleza fikra, busara na maono ya Hayati Karume.

Rais Mstaafu za Zanzibar, Dk. Ali Mohammed Shein, alisifu uwezo wa Hayati Karume hasa katika kuinua sekta ya elimu na utaalamu kwa Zanzibar akiwa na lengo la kuijenga Zanzibar mpya kitaaluma.

Alisema Hayati Karume alifanikisha hilo baada ya kutoa makundi ya Wazanzibari kuyapeleka kwenye mataifa ya kijamaa Ulaya na Amerika ikiwamo, Cuba, China, Bulgaria, Urusi na mataifa mengine kwa nia ya kujifunza na kurejesha Zanzibar uzoefu na maendeleo ya teknolojia.



Baadhi ya abiria wakikata tiketi kwenye kituo cha treni ya mwendo kasi mjini Morogoro kwa ajili ya usafiri wa kuelekea jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

# Wanahisa kupewa gawio la bil.1.8/-

**Na Gwamaka Alipipi**

WANAHISA kutoka kampuni ya usafirishaji mizigo (Swissport) wanatarajia kupata gawio la Sh. bilioni 1.8, baada ya kupatikana na faida ya Sh. bilioni 3.6 kwa mwaka 2023.

Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, Mrisho Yassin, alieleza hayo kwa waandishi wa habari jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano wa 39 wa wanahisa ambao ulikuwa na agenda ya kupitisha mahesabu ya mwaka 2023 pamoja na kugawa gawio kwa wanachama wake.

Yassin alisema faida ya kampuni kwa mwaka 2023 ilikuwa Sh. bilioni 3.6, hivyo wanahisa wa kampuni hiyo wanapewa asilimia 50 ya faida ambayo wameitengeneza kwa mwaka huo.

"Mwaka 2022 kampuni ilipata faida ya Sh. bilioni 2.6 na mwaka 2023 imepata ya Sh. bilioni 3.6 utaona hapa faida imeongezeka na hii imechangiwa na kuongezeka kwa miruko ya ndege, idadi ya mizigo ambayo tulihudumia katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere na Kilimanjaro iliongezeka hali ambayo ilisababisha kuongezeka kwa mapato yetu. Hata hivyo gharama zetu za uendeshaji hazikuongezeka," alisema.

Aidha, alisema kama kampuni wanatarajia kutanua huduma zao na wanaimani siku moja wataweza kutoa huduma katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume Zanzibar pamoja na viwanja vingine Afrika.

Alisema: "Jitihada za serikali ni kubwa katika kukuza utalii wa nchi na hii imesababisha kuongezeka kwa watalii na wageni wanaokuja Tanzania, hivyo mizigo pia imeongezeka hasa usafirishaji nje ya nchi," alisema.

Mmoja wa wanahisa wa kampuni hiyo, Aika Shauri, alisema mkutano huo ulikwenda vizuri na wanashukuru kwa gawio waliolipata na wanaona kampuni hiyo inaendelea kukua.

Mwanahisa mwingine, Irene Tarimo alisema kampuni hiyo inafanya vizuri hasa ya kuwasaidia wanachama wake kuweza kujikwamua kiuchumi.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**IN THE DISTRIC COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No. 8847 of 2024**
**In the matter of the estate of the late**

**ZAKARIA JOSEPH MAKWALA**
**of Mwaja within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by**

**ROSE ZAKARIA MAKWALA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules Gn. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 24th day of 6 2024

Dated at Dodoma this 22 day of 5....2024

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ALEX MATEI MSHANA**

anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **HAOJUE** yenye usajili namba **MC 409 CHY, CHASSIS** NAMBA: **LC6PCJK20K0056156** na ENGINE NAMBA: **156FM15AD2F56796.**

Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/RUV/SON/3229/2024**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 12940 OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late:**
**MASINDE NYANGERO**

**By 1: ALEXANDER NYANGERO SONGORWA**
**2: ________________________**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 27 day of JUNE.2024

Dated at Morogoro this 6 day of JUNE.2024

RESIDENT MAGISTRATE

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
P.O.Box 660, Morogoro

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**SHAD KREN MAKEVE**

anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji yenye usajili namba MC 601 DDH. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/NJO/NJO/2257/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**EDDA SAMWELY** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2492/0003** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MAWENGI SECONDARY SCHOOL TANZANIA** mwaka 2009. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: 30/3/8/17**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**LA WILAYA MPWAMPWA**
**LILILOKO DODOMA**
**MAOMBI NA. 06 YA MWAKA 2024**
**PETER LUMAMBO...............MDAI**
**VERSUS**
**ZAKAYO BENDERA...............MDAIWA**

**KWA:**
**ZAKAYO BENDERA**
**POPOTE ULIPO.**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Mpwapwa wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 23.07.2024 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANGALIZO:**- Kama hakuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/ Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 16 ya Mwezi wa APRIL, 2023.

..........................................................................

**MWENYEKITI**
**Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya**
**MPWAPWA.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PAUDOLA ZABRON PILLA**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA SCANIA YENYE USAJILI **T 879 DXZ** ,INJINI NAMBA **0620558460** CHASISI NAMBA **VLUR4X20009058460** , KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA

**PHQ/IRI/IRI/8528/2024.**

## KADI ZA GARI ZIMEPOTEA

**RORY MAXWELL NIGHTINGALE**

ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI ZA GARI T509BAF CHASSIS NAMBA -A0500419 ,ENGINE NAMBA CD4045G034268 T523BHL CHASSISS NAMBA H4432EAA0201942,ENGINE NAMBA CD6068G118902 YEYOTE ATAKAYEZIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI

**PHQ/ARU/ARU/ 20204/2024.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya MASWA.**
**Kituo cha NYALIKUNGU mkoa wa SIMIYU**
**Shauri la Madai Na.29/2024**
**Jina la Mdai KCCL KAHAMA Co L.T.D**
**Jina la Mdaiwa MISPINA KULWA NA WENZAKE WANNE.**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA.**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa EMILY KULWA WA BUGARAMA,MASWA**
**K.K: M/KITONGOJI BUGALAMA**
**K.K VEO BUGALAMA,MASWA**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba(Eleza hapa habari za Madai)Madi anawadai wewe pamoja na wenzako wanne pesa taslimu Sh 14,317,320/- baki ya pesa za ununuzi wa pamba. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 18 Mwezi 06 Mwaka 2024 saa 2;30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa sharini .Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.

Hati hii Imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 13 Mwezi 06 Mwaka 2024.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
NYALIKUNGU

## TANGAZO LA NOTISI WADAIWA

**TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICE LIMITED,** Inatangaza notisi kwa wadaiwa waliokopa mikopo na kushindwa kulipa madeni yao kama ifuatavyo:-

**WILLIAM PATRICK CHIBONI** - Mkoa Dar Es Salaam. Hii ni notisi ya siku thelathini (Siku 30) kutakiwa kulipa deni kwa kudhamini **GETRUDE ARCHARD NJAU.**

Mnatakiwa kulipa madeni yenu ya mikopo mnayodaiwa na Tujijenge ndani ya muda husika ulioainishwa mbele ya jina lako.

Hii ni baada ya mkopo kushindwa kulipwa kulingana na masharti na makubaliano ya mkataba.

Notisi hii itatumika kuanzia tarehe ya Tangazo hili gazetini. Hatua zaidi za Kisheria zitachukuliwa dhidi yako endapo kama utashindwa kulipa deni la mkopo ndani ya muda ulioainishwa/kutangazwa.

Ikiwa ni pamoja na kufuata taratibu nyingine za kisheria au kuruhusu dalali kuuza mali zilizotumika kudhamini mkopo uliochukuliwa.

**Kwa Mawasiliano piga:**
**+255 222774742-3/0677088251/0718068335**
**Au Email: tujijengetanzania@tujijenge.or.tz**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya MASWA.**
**Kituo cha NYALIKUNGU mkoa wa SIMIYU**
**Shauri la Madai Na.30/2024**
**Jina la Mdai KCCL KAHAMA Co L.T.D**
**Jina la Mdaiwa BENEDICTOR G.MAKUBI NA WENZAKE WANNE.**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA.**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa EZEKIEL G MAKUBI WA MWASAYI,MASWA**
**K.K: M/KITONGOJI MWAJIJABENDE**
**K.K VEO MWASAYI,MASWA**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba(Eleza hapa habari za Madai) Madi anawadai wewe pamoja na wenzako wanne pesa taslimu sh 21,973,880/- baki ya pesa za ununuzi wa pamba. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 18 Mwezi 06 Mwaka 2024 saa 2;30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea. **ANGALIZO:**Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa sharini .Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo. Hati hii Imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 13 Mwezi 06 Mwaka 2024.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
NYALIKUNGU

## OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

## MOB: +255 - 0677020701

## E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,

## WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**Piga Simu 0677020701**

## MNADA WA HADHARA

Madalali tajwa hapo chini tunatangazia umma kuwa kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana za wadaiwa kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utaendeshwa kwa idhini tuliyopewa na Tujijenge Tanzania Financial Service Ltd kama ilivyotangazwa gazetini,; Pia tunatoa notisi ya siku kumi na nne ya kulipa deni kwa mdaiwa, vinginevyo tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha gazetini

| Mdaiwa | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada | Dalali |
|---|---|---|---|
| Nicholas Ernest Mgaya | Gari T.525 CUP Toyota COASTER - Dalali Yard | 02/07/2024 | SEPCO Debt Collections & Auctioneering Co. Ltd |
| Fransisca Isaac Mwakajila | Gari T.224 EAU Toyota RACTIS -Mbagala yard | 05/07/202 | RAPITECH Solutions Ltd |
| Marco Lucas Lumashi | Nyumba ipo'Kisesa | 04/07/202 | JOSINA CO. LTD |

**Masharti Mengine:**

Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi na mnada utarudiwa tena. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**SEPCO: 0715683777 & JOSINA: 0768203040/0789203040**
**Tujijenge (T) Financial Services Ltd: 0718068335**
**RAPITECH Solutions Ltd: 0755264606**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji wa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

## Uamuzi wa hakimu wamsababishia kifo

**Nairobi,** KENYA

HAKIMU wa Kenya aliyepigwa risasi na ofisa mkuu wa polisi mapema wiki hii amefariki, kwa mujibu wa jaji mkuu wa nchi hiyo.

Jaji Martha Koome aliandika kwenye X, kwamba Hakimu Mkuu wa Mahakama ya Sheria ya Makadara, Monica Kivuti, ameshindwa katika vita, dhidi ya majeraha yake makubwa.

Kivuti alipigwa risasi na polisi katika mahakama moja katika mji mkuu, Nairobi, siku ya Alhamisi baada ya kufutilia mbali dhamana ya mkewe kutokana na kutoroka kwa mwanamke huyo.

Polisi huyo aliyetambulika kwa jina la Samson Kipchirchir Kipruto aliuawa kwa kupigwa risasi na maofisa wengine kufuatia shambulizi hilo.

Maofisa watatu kati ya hawa walijeruhiwa katika shambulio hilo lakini wanasemekana kuwa katika hali shwari.

„Ni kwa moyo mkunjufu ninalitaarifu taifa kuwa Monica Kivuti, Hakimu Mkuu, Mahakama ya Sheria ya Makadara, ameshindwa katika mapambano dhidi ya majeraha makubwa aliyoyapata wakati wa shambulio la wazi la bunduki mahakamani,“ alisema Jaji Koome katika taarifa yake Jumamosi.

„Familia ya Mahakama inasimama kwa mshikamano wakati huu wa kiwewe kikubwa na inataka usikivu na huruma tunaposhiriki katika huzuni.“

Kulingana na gazeti la The Star, lililozungumza na chanzo katika Hospitali ya Nairobi, Kivuti alifariki Ijumaa usiku baada ya kupigwa risasi kifuani na mguuni.

Mahakama za Sheria za Makadara zinapaswa kusalia kufungwa hadi Jumatatu.

Huduma ya polisi ya kitaifa ilisema katika taarifa siku ya Alhamisi kwamba Kipruto, ambaye alikuwa msimamizi wa kituo cha polisi cha Londiani magharibi mwa Kenya, alikuwa mahakamani kwa sababu zisizojulikana wakati wa kusikilizwa kwa kesi ya mkewe.

Alishtakiwa kwa kupokea pesa „chini ya udanganyifu.“

Uchunguzi wa kilichotokea unaendelea.

Jaji Koome alisema ni wazi kuwa Kipruto alinuia kumuua Kivuti.

Kisa hicho ndani ya chumba cha mahakama kimewashtua Wakenya.

Polisi mara nyingi wamekuwa wakishutumiwa kuhusika na mauaji ya nje ya mahakama, lakini hakuna tukio kama hilo lililoripotiwa ndani ya mahakama.

Mahakama imesema itaimarisha hatua za usalama na imewahakikishia wafanyakazi wa mahakama na watumiaji wengine wa mahakama usalama na usalama wao.

Chama cha Wanasheria Kenya, kilisema katika taarifa kwamba tukio hilo halikuwa tukio la pekee bali ni sehemu ya mwelekeo wa kutatiza wa ongezeko la vitisho na mashambulizi dhidi ya maofisa wa mahakama na mawakili.

„Migogoro ya kisheria inaweza kuwa na hisia nyingi, na hatari kwa maofisa wa mahakama na mawakili haziwezi kupunguzwa.“

Jumuiya hiyo iliongeza kuwa itafanya kazi na Jaji Koome, kutayarisha mikakati ya kina inayolenga kulinda mfumo wa haki na watendaji wake.

### BINTIMFALME:

# Kate hadharani miezi mitatu tangu aanze tiba ya saratani

**London,** UINGEREZA

BINTIMFALME wa Wales, Kate, ambaye yuko kwenye matibabu ya saratani, ameonekana kwenye gwaride kuashiria kupandishwa kwa bendera ya kifalme.

Hili ni tukio la kwanza la umma kuhudhuria tangu utambuzi wake na kujitangaza anaugua saratani ya tumbo, mapema mwaka huu.

'Duchess of Cambridge', alionekana kwenye gari lenye kioo la kifalme la Uingereza. Baadaye, kisha kuonekana pia kwenye Varanda la Jumba la Buckingham.

Katika taarifa iliyotolewa siku moja kabla, Kate alisema matibabu yake yalikuwa yanampa maendeleo mazuri na akatangaza kwamba atashiriki gwaride kwa heshima ya mfalme.

Lakini pia aliongeza kuwa tiba hiyo haijakamilika na itaendelea kwa miezi kadhaa zaidi.

“Bado kuna njia ndefu mbele,“ aliandika katika ujumbe wake uliowekwa kwenye mitandao yake ya kijamii.

Tangu bintimfalme huyo anayefahamika kama bintimfalme wa Wales, afichue utambuzi wake wa maradhi ya saratani katika video ya kibinafsi kwenye mitandao ya kijamii Machi, mwaka huu, hakujawa na habari mpya kuhusu afya yake kutoka kwa ufalme.

Ujumbe mpya wa bintimfalme unaambatana na picha mpya iliyopigwa nje ya nyumba yake, huko Windsor.

Bintimfalme, hata hivyo, anaonya kwamba habari yoyote njema kuhusu ugonjwa wake inapaswa kuchukuliwa kwa tahadhari.

“Mtu yeyote ambaye amepitia tiba ya mionzi 'chemotherapy' anajua kwamba kuna siku nzuri na mbaya,“ alielezea.

“Siku moja unahisi dhaifu, umechoka, na unapaswa kuuruhusu mwili wako kupumzika. Lakini siku inayofuata, unahisi kuwa na nguvu na unataka kutumia zaidi afya yako nzuri,“ Kate aliendelea.

“Ninajifunza subira, hasa katika hali ya kutokuwa na uhakika. Ninaichukua kila siku inavyokuja; ninasikiliza mwili wangu na kujipa muda unaohitajika sana wa kupona,“ aliongeza.



Bintimfalme Kate Middleton akiwa kwenye gari katika gwaride la kuinua bendera ya kifalme. **PICHA: BBC**

## Ramaphosa kutangaza Baraza la Mawaziri

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

CYRIL Ramaphosa anajiandaa kuunda Baraza la Mawaziri, baada ya Bunge la Afrika Kusini kumchagua tena, kuwa rais wa nchi hiyo.

Hiyo ni baada ya makubaliano ya kihistoria ya muungano kati ya chama tawala cha African National Congress (ANC) na vyama vya upinzani.

Serikali mpya ya umoja wa kitaifa inaundwa na ANC ya Ramaphosa, Muungano wa mrengo wa kati wa Democratic Alliance (DA) na vyama vidogo.

Katika hotuba yake ya ushindi, Ramaphosa alipongeza muungano huo mpya, na kusema wapigakura wanatarajia viongozi kuchukua hatua na kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya kila mtu katika nchi hiyo.

Makubaliano hayo yaliharakishwa katika siku moja katika siku ya hali ya juu ya kisiasa, ambayo ilisababisha Bunge kukaa hadi jioni, kwa kura kuthibitisha ni nani angeshika madaraka katika utawala mpya.

Hapo awali, makubaliano yaliafikiwa kufuatia wiki kadhaa za uvumi kuhusu nani ANC ingeshirikiana naye baada ya kupoteza wingi wake wa wabunge kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 30 katika uchaguzi wa mwezi uliopita.

Ilipata asilimia 40 ya kura, huku DA ikishika nafasi ya pili kwa asilimia 22.

Katibu Mkuu wa ANC, Fikile Mbalula, aliutaja mpango wa muungano kuwa „hatua ya ajabu“.

Ilimaanisha kuwa Ramaphosa, ambaye alichukua nafasi ya Jacob Zuma kama rais na kiongozi wa ANC kufuatia mzozo mkali wa madaraka mwaka 2018, aliweza kushikilia mamlaka.

Hatua inayofuata ni kwa Bw Ramaphosa kutenga nyadhifa za baraza la mawaziri, ambazo zitajumuisha wanachama wa DA.

Mkataba wa vyama vingi hauhusishi vyama viwili vilivyojitenga na ANC, na huenda vitanufaika iwapo vitashindwa kuleta uboreshaji wa kiuchumi unaodaiwa na wapigakura.

Lakini kura za maoni zinaonyesha Waafrika Kusini wengi wanataka muungano huo mkuu ambao haujawahi kushuhudiwa ufaulu.

## HABARI MICHEZO

MAZOEZI



Kocha wa Timu ya Watoto ya Soccer School inayolelewa na Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete, Seif Jamal (kushoto), akisimamia mazoezi ya watoto hao katika Uwanja wa Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# JKT YAVUNJA BENCHI LA UFUNDI

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya JKT Tanzania umevunja benchi lao la ufundi ili kujipanga upya kwa ajili ya msimu ujao wa 2023/2024 unaotarajiwa kuanza Agosti mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Masau Bwire, alisema wamechukua uamuzi huo baada ya kuona malengo yao hayajatimia msimu uliopita.

„Malengo yetu yalikuwa ni kushiriki mashindano ya Kimataifa msimu ujao lakini haikuwa hivyo, ndio maana tunataka tuwe na benchi bora la ufundi, alisema Masau.

Aidha, alisema hawakufurahishwa kuona timu yao inacheza mchezo wa mtoano kuwania kubaki Ligi Kuu na kiliwaumiza viongozi na mashabiki wao kwa kiasi kikubwa.

Vile vile alisema muda wowote kuanza sasa watatangaza benchi jipya la ufundi ambalo litaanza majukumu yake Julai mwaka huu.

„Hivi karibuni tutatangaza benchi letu jipya la ufundi ambalo litawajibika na timu msimu ujao, tunaamini litafanya mapinduzi makubwa, alisema.

Aidha alisema licha ya kuachana na benchi hilo bado wanahitaji ushauri na maoni kutoka kwa aliyekuwa kocha wao mkuu, Malale Hamsini ambaye ameacha ripoti yake.

Aliwataka mashabiki wao kuwa na subira kipindi hiki ambacho wanajiandaa kuwatangazia benchi jipya la ufundi.

# 'Miss Grand 2024' kushiriki shindano la dunia

**Na Shufaa Lyimo**

MSHINDI wa shindano la urembo la ‚Miss Grand 2024' atapata fursa ya kushiriki shindano la dunia litakalofanyika Oktoba mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana wakati wa uzinduzi wa ‚Miss Grand', mwandaaji wa shindano hilo Nazimizye Ada Mdolo alisema mshindi wa kwanza katika shindano hilo atapata fursa ya kwenda kushiriki mashindano ya Dunia Oktoba 25 mwaka huu nchini Myanmar.

Alisema mshindi wa pili kwenye shindano hilo atapata fursa ya kwenda kushiriki mashindano ya Afrika ambayo yatatangazwa baadaye.

„Hili ni shindano kubwa ambalo linakwenda kutangaza utalii wa nchi yetu vile vile linasaidia wasichana wengi kupata ajira, alisema, Ada Mdolo.

Alisema analishukuru Baraza la Sanaa la Taifa (Basata) kwa kuwapa kibali cha kuandaa shindano hilo na kuwataka wasichana wajitokeze kuchukua fomu za ushiriki ambazo zitaanza kupatikana hivi karibuni.

Kwa upande wake Mratibu wa Shindano hilo, Tumaini Henry, aliwataka wasichana wajitokeze kuchukua fomu hizo na kudai mwaka huu shindano hilo mwaka huu litakuwa na ubora z a i d i tofauti lililofanyika mwaka 2018.

Wakati huo huo aliyekuwa ‚Miss Grand Tanzania 2018', Queen Mugesi, alisema kupitia shindano hilo amejifunza vitu vingi ikiwa pamoja na kupata mawasiliano na watu kutoka nchi mbalimbali.

„Nilipata fursa ya kutembelea nchi mbalimbali kupitia shindano hili, vile vile niliweza kufanya kazi na taasisi tofauti tofauti, ninashukuru kwa hatua niliyofikia, alisema Mugesi.

Vile vile Daxx Cruz ambaye ni miongoni mwa waandaaji alisema vigezo vya washiriki ni msichana mwenye umri kuanzia miaka 18-29 ambapo wanataka kuwainua watoto wa kike.

# Ligi Mabingwa Wanawake kutimua vumbi Dodoma

**Na Adam Fungamwango**

LIGI ya Mabingwa wa Mikoa katika soka la Wanawake inatarajiwa kuanza kupigwa Jumatano Juni 19 mpaka 29 kwenye Uwanja wa Shule ya Fountain Gate jijini Dodoma.

Taarifa iliyotolewa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), ikisainiwa na Ofisa Habari na Mawasiliano, Cliford Ndimbo, imesema jumla ya timu 19 ambazo ni mabingwa kutoka katika mikoa mbalimbali nchini zinatarajiwa kuonyeshana kazi ambapo mwisho wake itatoa timu mbili za juu ambazo zitapanda na kucheza Ligi Daraja la Kwanza (WFDL) kwa msimu wa 2024/25.

TFF, imezitaka timu zote kufika kituoni Juni 18, tayari kwa kuanza kinyang'anyiro hicho.

Timu ambazo tayari zimepata nafasi hiyo na zimethibitisha kushiriki, majina ya mikoa yao ikiwa kwenye mabano ni Mbagala Queens (Dar es Salaam), Mayai Sport (Morogoro), Singida Rising Star (Singida), Ziba Sekondari (Tabora), Nguruka Princess (Kigoma), Katoro Princess (Geita), TSC Queens (Mwanza), Bunda Girls (Mara), na Raha Queens (Simiyu).

Timu zingine ni Kitwana Princess (Shinyanga), Lengo Queens (Arusha), Simba Footprint (Kilimanjaro), Leopards Princess (Tanga), Chipuputa Queens (Mtwara), Tutes Queens (Ruvuma), Michael Jackson Princess (Njombe), Veta Iringa Ladies (Iringa), Prisons Queens (Mbeya) na Maendeleo Queens (Songwe).

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**MAN YAKOMAA NA LIGT**

KLABU ya Manchester United imeanza mazungumzo kuhusu uhamisho wa beki wa Bayern Munich, Mholanzi Matthijs de Ligt mwenye umri wa miaka 24, ambaye ana thamani ya takribani euro milioni. (***Sky Sport Germany***)

**BEI YA BRANTHWAITE YAKATALIWA**

MANCHESTER United haina nia ya kufikia thamani ya Everton ya pauni milioni 70 kumnunua mlinzi, Jarrad Branthwaite mwenye umri wa miaka 21. ***(Mirror)***

**WALSH ATAKIWA ARSENAL**

KLABU ya Arsenal ina nia ya kutaka kumnunua kiungo wa kati wa Barcelona, Keira Walsh mwenye umri wa miaka 27. (***Athletic***)

**GREENWOOD KUBAKI HISPANIA**

VALENCIA imewasilisha ombi la pauni milioni 25 kumnunua mshambuliaji wa Manchester United, Mason Greenwood mwenye umri wa miaka 22, huku mshambuliaji huyo wa England, ambaye amekuwa akihusishwa na Juventus akitaka kusalia Hispania baada ya kucheza kwa mkopo Getafe msimu uliopita. (***Mirror***)

**GREALISH KUONDOKA**

MLINZI wa England, Jack Grealish mwenye miaka 28, anaweza kutaka kuondoka Manchester City baada ya kukosa nafasi katika kikosi cha kwanza msimu uliopita lakini mshahara wake mkubwa na mkataba wake hadi 2027 unaweza kuwa kikwazo. (***Football Insider)***

**BROJA AWANIWA MILAN**

AC Milan ilituma skauti kumtazama Armando Broja mwenye umri wa miaka 22, akiichezea Albania dhidi ya Italia Jumamosi huku klabu hiyo ya Serie A ikitathmini uwezekano wa kumnunua mshambuliaji huyo wa Chelsea. ***(Sky Sports Italia)***

**LILLE YAKATAA KUMUUZA YORO**

KLABU ya Lille imekataa dau la pauni milioni 42.3 kutoka kwa klabu ambayo haijatajwa jina kwa mlinzi wa kati, Leny Yoro mwenye umri wa miaka 18, ambaye amekuwa akihusishwa na kutaka kuhamia Liverpool na Manchester United lakini inasemekana anapendelea uhamisho wa kwenda Real Madrid. (***Express***)

**LINDELOF ALENGWA**

MLINZI wa Manchester United, Victor Lindelof mwenye umri wa miaka 29, analengwa na kocha mpya wa Fenerbahce, Jose Mourinho, ambaye alifanya kazi na mchezaji huyo wa Sweden wakati alipokuwa Old Trafford. (***Fotomac***)

**ADEJENUGHURE AWINDWA**

KLABU ya Manchester United imeungana na AC Milan na Borussia Dortmund kumwinda mshambuliaji wa RB Salzburg, Oghenetejiri Adejenughure mwenye umri wa miaka 17, ambaye alifunga mabao manne katika michezo minne akiwa na Austria wakati wa michuano ya hivi karibuni ya Ulaya kwa vijana chini ya umri wa miaka 17. ***(Express)***

**MASTANTUONO ANYATIWA MAN**

KLABU ya Manchester City inalenga kuteka uhamisho wa Real Madrid kwa kiungo wa kati wa River Plate Muargentina Franco Mastantuono mwenye umri wa miaka 16, ambaye ana kipengele cha kuachiliwa cha pauni milioni 45. ***(Sport via 90 Min)***

**ANTON AWANIWA LIVERPOOL**

KLABU ya Liverpool ilifanya uchunguzi kuhusu mlinzi wa kati wa Stuttgart, Waldemar Anton mwenye umri wa miaka 27, ambaye yuko kwenye kikosi cha Ujerumani kwenye Euro 2024 na ana kipengele cha kutolewa cha euro milioni 22.5. ***(Sport Bild***)

**SANCHO SASA ATAKIWA JUVE**

KLABU ya Juventus imesonga mbele ya Borussia Dortmund katika kujaribu kumsajili winga wa Manchester United, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 24, ambaye alitumia kipindi cha pili cha msimu uliopita kwa mkopo katika klabu hiyo ya Ujerumani. (***Football Insider***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# DECO ATAKA RAPHINHA ABAKI BARCELONA

**BARCELONA,** Hispania

### ●●● Nyota huyo anatwaja kutaka kuuzwa ili kuepusha matatizo zaidi ya...

MKURUGENZI wa Michezo wa Barcelona, Deco anatamani kuona Raphinha akisalia katika klabu hiyo licha ya uvumi unaomuhusisha winga huyo kutaka kuondoka.

Miamba hao wa Hispania watahitaji mauzo msimu huu wa majira ya joto ikiwa wanataka kuepusha matatizo zaidi ya kifedha.

Mmoja wa wachezaji wanaotajwa kuuzwa ni nyota wa Brazil, Raphinha.

**Lakini kwa mujibu wa Sport, Deco hataki kutengana na mchezaji huyo hata ikiwa wanataka kununua wachezaji wapya.**

Ripoti hiyo inaendelea kusema kuwa Deco, ambaye aliwahi kuwa wakala wa Raphinha kabla ya kujiunga na Barcelona, hataki kumlazimisha mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil kuhamia Saudia, ambapo klabu ziko tayari kutoa kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya winga huyo.

Iwapo Raphinha atasalia na Barcelona, maswali yatabaki juu ya jukumu lake.

Alicheza mechi 17 tu kwenye LaLiga msimu uliopita, huku Xavi akimpendelea Lamine Yamal anayeibukia katika nafasi yake badala yake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 bado ana pale mkataba Camp Nou hadi 2027 na amekuwa akiweka wazi mara kwa mara kuwa hataki kuondoka.

Bila kumuuza Raphinha, Barcelona hawataweza kugharamia uhamisho wa winga mwingine, huku Nico Williams wa Athletic Club akitajwa kuwa ndiye anayependelewa ikiwa fedha za kutosha zitapatikana.

Kwa sasa Raphinha yuko na timu ya taifa ya Brazil kujiandaa na Copa America.

Kocha mpya Hansi Flick atataka kuzungumza na winga huyo na kuthibitisha mipango yake ya msimu ujao.

HABARI MICHEZO

# YAMAL AWEKA REKODI EURO



**BERLIN,** England

NYOTA wa Barcelona, Lamine Yamal amekuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuwahi kushiriki michuano ya Ulaya katika ushindi wa Hispania dhidi ya Croatia mjini Berlin Jumamosi.

Akiwa na umri wa miaka 16 na siku 338, Yamal amefuta rekodi ya kiungo wa kati wa Poland, Kacper Kozłowski, ambaye alikuwa na umri wa miaka 17 na siku 246 alipotoka kwenye benchi kwenye Euro 2020 (ambayo ilichezwa 2021 kutokana na janga la COVID-19) dhidi ya Hispania.

Hiyo ilikuwa mara ya pili katika michuano hiyo rekodi hiyo kushuka, huku Muingereza Jude Bellingham akiwa amepandisha daraja iliyowekwa na beki wa kushoto wa Uholanzi Jetro Willems kwenye Euro 2012.

„Anaendelea tu kuvunja rekodi," alisema Kocha wa Hispania, Luis de la Fuente kuhusu Yamal katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mchezo. „Anakua, anakomaa na anakuwa bora kila siku.

„Yuko kwenye njia ya kuwa mchezaji mkubwa, lakini ni mdogo sana na tunapaswa kuwa na subira naye."

Yamal aliifungia Hispania bao la tatu katika ushindi wa 3-0 dhidi ya Croatia na kutoa krosi bora kwa Dani Carvajal huku mabingwa hao mara tatu wakianza michuano wao kwa mwanzo bora zaidi.

„Nina furaha sana kwa ushindi huo, kwa mechi ya kwanza na sasa tunabadilisha mtazamo wetu hadi mchezo unaofuata," Yamal alisema baadaye.

„Mwishowe, timu inataka kucheza ndani na niko hapa kusaidia timu, kulinda, chochote kinachohitajika.

„Sisi ni timu yenye ufanisi sana kwa sababu kazi ambayo tumeweka katika miezi michache iliyopita imeonekana leo."

Wakati Yamal akiwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuwahi kucheza katika historia ya Euro, bao la Carvajal lilimfanya kuwa mfungaji bora zaidi wa Hispania katika mashindano hayo akiwa na umri wa miaka 32.

Nahodha Álvaro Morata na Fabian Ruiz pia walifungia Hispania ilipo songa mbele katika kipindi cha kwanza, lakini walichanganyikiwa katika kipindi cha pili ambacho hakikuwa na matokeo.

Vonlanthen wa Uswisi alikuwa na umri wa miaka 18 na siku 141 alipotikisa nyavu kwenye michuano ya Euro 2004, siku nne tu baada ya Muingereza Wayne Rooney kuwa mfungaji mwenye umri mdogo zaidi katika michuano ya Ulaya.

Wakati huo huo, Bellingham ndiye mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuwahi kucheza mchezo wa mtoano akiwa na miaka 18 na siku nne, mdogo kidogo kuliko Pedri wa Hispania na Jamal Musiala wa Ujerumani walikuwa kwenye dimba moja, Euro 2020.

Renato Sanches wa Ureno ndiye mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kucheza fainali akiwa na umri wa miaka 18 na siku 328 -- Yamal atafikisha miaka 17 siku moja kabla ya fainali mjini Berlin.

Winga wa Barca Yamal tayari ndiye mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuanza na kufunga katika LaLiga, huku pia akiwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kutokea katika mchezo wa mtoano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya mapema mwaka huu dhidi ya Napoli.

# Spalletti asifu kikosi cha Italia



**DORTMUND,** Ujerumani

KOCHA wa Italia, Luciano Spalletti amesema timu yake „ilizima" kwa bao la rekodi la mapema la Albania, lakini akasifu jinsi ilivyojizatiti na kupata ushindi wa 2-1 kwenye mechi yao ya ufunguzi ya Euro 2024 huko Dortmund Jumamosi.

Italia waliingia uwanjani wakiwa mabingwa watetezi na Spalletti alisema ni lazima timu yake iwe ya bora zaidi mbele ya lango ikiwa wanataka kutetea ubingwa huo.

Mabao kutoka kwa Alessandro Bastoni na Nicolò Barella yalitosha kuipa Italia pointi tatu baada ya hofu ya mapema.

Albania, iliyochangiwa na mashabiki angalau theluthi mbili ya uwanja, iliweka historia ya Euro wakati Nedim Bajrami alipofunga bao la haraka zaidi katika historia ya mashindano baada ya sekunde 23.

Bao lilitokana na makosa ya Federico Dimarco alipiga mpira wa kurusha upande wa kushoto na Bajrami akauwahi na kumfunga, Gianluigi Donnarumma.

"Mambo haya yanaweza kutokea kwa sababu tulizima," alisema Spalletti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Lakini tunahitaji kuthamini nia ya kujaribu na kwenda kucheza mpira hata wakati hali ilipokuwa ngumu.

"Tulihitaji tu kuweka mambo vizuri na nadhifu hapo, kama tulivyowekwa ndani."

## Ronaldinho akanusha kuiponda Brazil

**RIO DE JANEIRO,** Brazil

GWIJI wa soka wa Brazil, Ronaldinho amesema shutuma zake kwa kikosi cha mwaka huu cha timu ya taifa ya Brazil kwenye michuano ya Copa America ni mkusanyiko wa ‚maoni' yaliyotolewa na mashabiki kwenye mitandao ya kijamii ambayo aliyatoa kama sehemu ya kampeni ya kutangaza bidhaa ya kuondoa harufu kwenye mawili.

Hapo awali Ronaldinho alikuwa amechapisha kwenye Instagram kwamba kuna „ukosefu wa upendo kwa jezi ya Brazil" miongoni mwa wachezaji akiwamo Raphinha.

Hata hivyo, saa chache baadaye, Ronaldinho alisema maneno hayo si yake na alikuwa akijaribu kuunga mkono upande wa sasa.

„Sitaacha kamwe kuiunga mkono Brazil," aliandika kwenye akaunti yake ya Instagram.

„Uungwaji mkono wa mashabiki unaleta mabadiliko makubwa kwa wachezaji na wanachohitaji ni kuungwa mkono kwa wakati huu," aliendelea kusema.

Ronaldinho, ambaye alishinda Copa América akiwa na Brazil mwaka 1999 na Kombe la Dunia mwaka 2002, awali alionekana kuishutumu Brazil.

„Ni vigumu kupata nishati kutazama michezo," aliandika. „Hii labda ni moja ya timu mbaya zaidi katika miaka ya hivi karibuni, haina viongozi wa heshima, ni wachezaji wa wastani kwa sehemu kubwa.

„Nimekuwa nikifuatilia soka tangu nikiwa mtoto, muda mrefu kabla sijafikiria kuwa mchezaji, na sijawahi kuona hali mbaya kama hii. Kuna ukosefu wa upendo kwa jezi, ukosefu wa dhamira na mengi zaidi.

„Uchezaji umekuwa moja ya mambo mabaya zaidi ambayo nimewahi kuona. Ni aibu. Ndio maana natangaza kuwa ninakata tamaa hapa. Sitatazama mechi yoyote ya Copa América na sitashangilia ikiwa Brazil itashinda."

Mechi ya kwanza ya Brazil katika Copa América inakuja dhidi ya Costa Rica mnamo Juni 24, huku Colombia na Paraguay pia zikiwa Kundi D.



## HABARI MICHEZO

### Dewji ambakisha Ayoub Simba

INATOKA UK. 24

juu na kushangaza wengi.

Hadi Ligi Kuu msimu uliomalizika unafikia ukingoni, alikuwa ndiye kipa namba moja wa timu hiyo, ambapo nafasi hiyo hauikuja hivi hivi bali kazi kubwa aliyokuwa akiifanya ya kuokoa michomo ya hatari kutoka kwa wapinzani waliokuwa wakicheza dhidi ya timu hiyo, hasa katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi Kuu Tanzania Bara.

„Hatukuwa vizuri msimu uliomalizika, lakini kipa huyu alitusaidia sana, alikuwa na kiwango kikubwa mno, aliangushwa na safu ya ulinzi, kiungo mkabaji, na timu nzima kwa ujumla, sasa kwa usajili huu unaoendelea nafikiri atakuwa kwenye kiwango bora zaidi kuliko hata cha msimu uliopita," kilisema chanzo hicho.

Baada ya kumalizika kwa mchezo wa mwisho wa Ligi Kuu dhidi ya JKT Tanzania, Mei 28, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Ayoub alionekana kuwaaga mashabiki wa klabu hiyo waliokuwa wamekaa jukwaani na kutoa ishara kuwa anaondoka ndani ya klabu hiyo.



# COASTAL UNION KUMPIMA DJUMA SHABAN KAGAME

**Na Faustine Feliciane**

UONGOZI wa klabu ya Coastal Union umepanga kutumia mashindano ya Kagame Cup yatakayofanyika hivi karibuni kama maandalizi ya kushiriki Kombe la Shirikisho Afrika huku pia wakitumia kumpima beki Djuma Shaaban.

Coastal tayari imefanya mazungumzo na mchezaji huyo wa zamani wa Yanga na watampa mkataba wa kuitumikia timu hiyo msimu ujao.

**Mmoja wa viongozi wa klabu hiyo aliiambia Nipashe kuwa wame furahia kushiriki mi chuano ya Kagame msimu huu kwa kuwa yatakuwa sehemu ya maandalizi yao kabla ya kushiriki Kombe la Shirikisho Afrika.**

„Tumeyapokea mashindano hayo kwa fikra chanya, kwetu sisi itakuwa sehemu ya maandalizi ya michuano ya CAF, tutapata mechi za kimataifa kujipima," alisema kiongozi huyo ambaye hakutaka kutwajwa jina lake.

Aidha, alisema tayari wameshamalizana na Djuma lakini watayatumia mshindano hayo ya Kagame kama kipimo kwake kuona kama atawasaidia.

„Kila kitu kipo sawa, tumeshakubaliana naye, lakini mashindano ya Kagame ni kipimo kwake kuona nini ambacho atakiongoza kwenye kikosi chetu," alisema kiongozi huyo.

Coastal Union itaiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kumaliza Ligi Kuu ikiwa kwenye nafasi ya nne nyuma ya wawikilishi wenza, Simba.



Djuma Shaaban, beki wa zamani wa Yanga anayetajwa kujiunga na Coastal Union ya Tanga kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu na mashindano ya Kimataifa. **PICHA: MTANDAO**

# Tabora United yabaki Ligi Kuu Bara

**Na Faustine Feliciane**

TIMU ya Tabora United imenusurika kushuka daraja baada ya jana kupata ushindi muhimu wa mabao 2-0 dhidi ya Biashara United katika mchezo wa marudiano wa mchujo wa mwisho wa kuwania kubaki Ligi Kuu Tanzania Bara kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mjini Tabora.

Tabora walikuwa wanahitaji ushindi huo muhimu kuweza kubaki Ligi Kuu baada ya kupoteza mchezo wa kwanza kwa bao 1-0.

Shujaa wa Tabora United alikuwa mshambuliaji wa Kimataifa wa Angola, Patrick Lembo Aufumu aliyefunga mabao yote mawili, la kwanza kwa penaltı dakika ya 27 na bao la pili dakika ya 55 akimalizia mpira wa adhabu ndogo.

Kwa matokeo hayo, Tabora United inaitoa Biashara United kwa ushindi wa jumla wa 2-1 na kuifanya timu hiyo isalie Ligi ya ‚Championship' kwa msimu ujao.

Ikumbukwe Biashara United imetoka ligi hiyo na imecheza hatua ya mtoano baada ya kuifunga Mbeya kwanza kabla ya kukutana na Tabora United iliyotoka kupoteza mbele ya JKT Tanzania kwenye mchezo wa kwanza wa ‚Play Off' kwa timu za Ligi Kuu.



# Michezo

Nipashe

Jumatatu Juni 17, 2024




Deco ataka Raphinha abaki Barca UK. 21



## Dewji ambakisha Ayoub Simba

**Na Mwandishi Wetu**

MWEKEZAJI, Rais wa Heshima na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya klabu ya Simba, Mohamed Dewji, amefanikiwa kumbakisha golikipa namba moja wa timu hiyo kwa sasa, Ayoub Lakred kwa kumwongezea mkataba wa mwaka mmoja.

Taarifa za uhakika zilizopatikana jana zinasema kuwa kipa huyo ambaye tayari alikuwa amemaliza mkataba wake wa msimu mmoja na hakutaka kuendelea tena na timu, amebadili mawazo baada ya mazungumzo ya kina na Mo mwenyewe ambaye amemshawishi hadi kufikia hatua hiyo.

„Ayoub amebaki, juzi amesaini tena mkataba wa mwaka mmoja, sasa anakaa hadi Juni 2025, bosi Mo ndiye aliyembadili mawazo. Hakutaka tena kuendelea kuitumikia Simba, kuna klabu kadhaa Misri, kwao Morocco na Tunisia zilikuwa zinamhitaji, ikiwamo FAR Rabat ambako alitoka, kwa hiyo bado tunaye,“ kilisema chanzo chetu ndani ya klabu hiyo.

Alisema mazungumzo hayo yalifanyika kwa njia ya simu, na si kwamba alikwenda Dubai, Falme za Kiarabu kukutana na Mo kama inavyozungumzwa.

Mtoa taarifa huyo alisema kwa sasa Ayoub yuko nchini kwao Morocco akipumzika na familia yake.

Kipa huyo alisajiliwa na Simba mwanzoni mwa msimu uliopita, ambapo hakuwa na wakati mzuri mwanzoni, mashabiki wa timu hiyo wakiona kama hawakupata mtu sahihi wa kushindana na Aishi Manula, lakini muda mchache alibadilika baada ya kile kinachoelezwa kuzoea hali ya hewa na mazingira, akawa kwenye kiwango cha hali ya

INAENDELEA UK. 23

# Mukoko: Yanga bingwa tena 2024/2025

## ●●● Nyota huyo wa zamani wa Wanajangwani amesema kama klabu hiyo itabaki na...

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI wa zamani wa klabu ya Yanga, Mukoko Tonombe, ameitabiria timu hiyo kufika fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao kama itaendelea kuwa na asilimia kubwa ya wachezaji waliokuwa nao msimu uliomalizika.

Tonombe alisema kuwa klabu hiyo kwa sasa inatakiwa kuongeza tu baadhi ya wachezaji wachache wenye ubora kwa ajili ya kukiimarisha kikosi hicho.

Akizungumza juzi jijini Dar es Salaam, Tonombe, aliyeichezea Yanga kuanzia 2020 hadi 2022, amesema wala hatoshangaa kuiona timu hiyo ikifika fainali msimu ujao kama itaendelea kuwa na kina Stephane Aziz Ki, Maxi Nzengeli, Yao Kouassi, Djigui Diarra, Pacome Zouzoua na wengine ambao itawaongeza watakaokuwa nsa ubora zaidi.

Alisema kwa sasa Yanga ina wachezaji wengi bora zaidi kuliko walivyokuwa wao ndani ya kikosi hicho.

„Nimeona timu yangu ya zamani, wamechukua wachezaji wenye viwango vikubwa zaidi, walisajili wazoefu wa michezo ya kimataifa ndiyo maana wamewasaidia kufika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa na hili lilikuwa jambo bora zaidi.

Kama wataendelea na asilimia kubwa ya wachezaji hawa wa msimu uliopita, na wakaongeza wengine ambao wana viwango sawa nao au kuzidi, naiona msimu ujao ikifika fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wala haina shaka kabisa,“ alisema mchezaji huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Yanga ilifika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliomalizika, ikatolewa kwa mbinde na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini kwa mikwaju 3-2 ya penalti, baada ya timu hizo kucheza mechi nyumbani na ugenini bila kufungana ndani ya dakika 90.

Akizungumza kuhusu soka la Tanzania, Tonombe alisema kwa sasa limekua sana, huku akikiri kuumizwa mno alipoachwa na klabu ya Yanga, 2022.

Nimemisi sana maisha ya soka la Tanzania, nilivyoondoka Yanga niliumia sana, sababu kubwa ni kwamba mashabiki wa hapa wanapenda sana mpira, pili ni sehemu nzuri tulivu na ndiyo maana nimekuja tena hapa nchini,“ alisema.

Kiungo huyo mkabaji alisema kwa sasa amemaliza mkataba na TP Mazembe, na ana ofa nyingi mkononi, na muda si mrefu mashabiki wote watajua anaelekea wapi.

„Maisha ndivyo yalivyo, nimecheza Yanga nimetoka hapa, nimekwenda TP Mazembe, kwa sasa kule mkataba wangu umeisha, nimekuja Tanzania kuangalia marafiki zangu, familia ya mke wangu na Watanzania kwa ujumla.

Ni kweli nina ofa nyingi sana, utaona tu pale nitakapotua msimu ujao, nilimisi sana maisha ya Tanzania, kwangu naona mazuri mno,“ alisema mchezaji huyo.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >